**5 JUNI, 2026**

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA TATU

### Kikao cha Arobaini na Nne — Tarehe 5 Juni, 2026

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Mussa A. Zungu) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Katibu.

**NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:**

**KIAPO CHA UAMINIFU NA AHADI YA UZALENDO**

**SPIKA:** Kiapo cha Uaminifu.

**NDG. AZIZA WAZIRI KHEIR – KATIBU WA MEZANI:**

Mhe. Emmanuela Kaganda Mtatifikolo

*(Mbunge aliyetajwa hapo juu Aliapa Kiapo cha Uaminifu na Ahadi ya Uzalendo)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Maelezo ya Spika kuhusu kitendo cha Mheshimiwa Lucy Mayenga, Mbunge kutumia lugha isiyo ya Kibunge tarehe 21 Mei, 2026.

Waheshimiwa Wabunge, tarehe 21 Mei, 2026 Mheshimiwa Sigrada Wilhem Mligo, Mbunge aliomba ruhusa ya kiti ili kutoa taarifa. Taarifa hiyo ilieleza kuwa Mheshimiwa Lucy Mayenga

aliyekuwa anachangia bajeti ya Wizara ya Ujenzi. Kabla kiti kutoa uamuzi wa ombi hilo Mheshimiwa Lucy Mayenga alitamka maneno yafuatayo; “Mheshimiwa Naibu Spika, sitaki taarifa zako na wewe hebu kaa chini.”

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Sigrada aliendelea kuomba ruhusa ambapo kiti kilimpa nafasi na alipopewa nafasi alieleza yafuatayo; “Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, ninapenda kumpa taarifa mzungumzaji kwamba yeye siyo mamlaka ya kuzungumzia Serikali. Itakuja itazungumza yenyewe, yeye azungumze matatizo yake na asitushawishi.”

Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa Kanuni ya 80 ya Kanuni za Kudumu za Bunge 2025 Mheshimiwa Naibu Spika alimuuliza Mheshimiwa Mayenga kama anapokea au hapokei taarifa hiyo. Mheshimiwa Mayenga alijibu yafuatayo: “Mheshimiwa Naibu Spika, huyu hajitambui. Huyu hata kumjibu nitapoteza muda. Ninataka nizungumze jambo moja, ni kwamba...”

Waheshimiwa Wabunge, kutokana na maneno hayo kiti kilimtaka Mheshimiwa Mayenga azingatie kanuni kuhusu taarifa. Baada ya maelekezo hayo ya Naibu Spika, Mheshimiwa Mayenga alijibu: “sipokei.”

Waheshimiwa Wabunge, kutokana na tukio hilo Mheshimiwa Ado aliomba Mwongozo wa Spika chini ya Kanuni ya 79 ya Kanuni za Bunge. Mheshimiwa Ado aliuliza iwapo inaruhusiwa Mbunge kusema Bungeni kwamba Mbunge mwingine hajitambui.

Waheshimiwa Wabunge, kwa Kanuni ya 74(1)(j) inayokataza Mbunge kumsema vibaya Mbunge mwingine.

Waheshimiwa Wabunge, pamoja na kuwa kiti kilitoa mwongozo wa jambo hili tarehe 21 Mei 2026 imeona ipo haja ya kusisitiza kuhusu masharti ya kanuni inayokataza matumizi ya lugha isiyo ya Kibunge.

Waheshimiwa Wabunge, Kanuni ya 74(1)(j) na (k) inakataza Mbunge kutoa lugha ya matusi au ishara inayoashiria matusi,

kutumia lugha ya kudhalilisha au kumsema vibaya Mbunge au mtu mwingine.

Waheshimiwa Wabunge, masharti ya kanuni hii yanalenga kuhakikisha mijadala ya Bunge inafanyika kwa staha ili kulinda hadhi ya heshima ya Bunge.

Waheshimiwa Wabunge, maneno aliyotumia Mheshimiwa Lucy Mayenga, Mbunge tarehe 21 Mei 2026 kuwa Mbunge hajitambui ni lugha ya kuudhi, kudhalilisha, na kusemwa vibaya Mbunge mwingine.

Waheshimiwa Wabunge, aidha Mheshimiwa Mayenga alitumia maneno yafuatayo: "Mheshimiwa Naibu Spika, sitaki taarifa zako na wewe hebu kaa chini."

Waheshimiwa Wabunge, maneno hayo hayaoneshi heshima kwa kiti kilichokuwa kinaongoza kikao wala kwa Mbunge aliyeomba nafasi ya kutoa taarifa. Ikumbukwe kwamba kabla kiti hakijatoa uamuzi wa ombi la Mheshimiwa Sigrada, Mheshimiwa Lucy Mayenga aliingilia kati kwa kutumia lugha niliyoitaja hapo juu.

Waheshimiwa Wabunge, kutoheshimu kiti na kutumia lugha isiyo ya Kibunge ni ukiukwaji wa Kanuni za Bunge zinazosimamia majadiliano Bungeni. Hivyo ninatoa onyo kwamba maneno ya vitendo hivyo visirudiwe ndani ya Bunge. Hivyo, ninaelekeza kwamba maneno yafuatayo ya Mheshimiwa Lucy Mayenga yafutwe kwenye *Hansard:* "Mheshimiwa Naibu Spika, sitaki taarifa zako na wewe hebu kaa chini, na Mheshimiwa Naibu Spika, huyu hajitambui, huyu hata kumjibu nitapoteza muda."

Waheshimiwa Wabunge, niwakumbushe kwamba tarehe 18 Mei, 2026 nilitoa mwongozo na kusisitiza kuhusu umuhimu wa Wabunge kutumia lugha ya Kibunge katika mijadala yao. Pamoja na kufanya hivyo bado ya ukiukwaji wa kanuni unaendelea kujitokeza katika mijadala ya Wabunge.

Waheshimiwa Wabunge, kwa mara nyingine nitumie nafasi hii kuelekeza Wabunge wowote kuzingatia Kanuni ya 74

inayoweka masharti kuhusu mambo yasiyoruhusiwa Bungeni. Kanuni hiyo pamoja na mambo mengine inazuia:-

(a) Mbunge kutoa taarifa ambazo hazina ukweli, kumzulia jambo ambalo halipo kwenye mjadala;

(b) Kutotumia jina la Rais kwa dhihaka;

(c) Kutokutumia jina la nchi au kiongozi wa nchi nyingine kwa dhihaka; na

(d) Kutokutumia lugha ya matusi, kuuudhi au kumsema Mbunge mwingine vibaya au kufanya kitendo cha ujeuri au uchokozi.

Waheshimiwa Wabunge, matumizi ya lugha isiyo ya Kibunge hayakubaliki na kwa sababu yanaathiri utekezaji wa majukumu ya Kibunge. Hivyo, hatua zitachukuliwa kwa yeyote atakayekiuka masharti ya kanuni.

**SPIKA:** Katibu.

**NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**SPIKA:** Maswali, Ofisi ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Kassim Hassan Haji.

Waheshimiwa leo hamjapiga makofi? *(Makofi)*

Kanuni hizi ni za Kibunge, si za vyama na sisi tuna haki ya kuzifuata Kanuni za Kibunge sababu humu ndani tunafanya kazi za wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Kassim Hassan Haji.

Na. 518

**Kuondoa Changamoto Mfuko wa Jimbo**

**MHE. KASSIM HASSAN HAJI** aliuliza: -

Je, lini Serikali italeta narekebisho ya sheria ili kuondoa changamoto zinazoendelea katika utekelezaji wa Mfuko wa Jimbo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, ahsante sana na kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Kassim Hassan Haji, Mbunge wa Jimbo la Mwanakwerekwe kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo ulianzishwa kwa nia ya kuchochea shughuli za maendeleo katika jimbo. Madhumuni ya mfuko huu ni kuwawezesha Wabunge, kupitia Kamati za Mfuko wa Maendeleo ya Jimbo kuchangia shughuli za miradi ya maendeleo inayobuniwa na wananchi katika Mpango wa Fursa na Vikwazo *(O&OD)* na kuidhinishwa na halmashauri.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza azma hii, mwaka 2009 Bunge lako lilitunga Sheria ya Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo *(The Constituencies Development Catalyst Fund Act)* Sura ya 96 ambayo imeanzisha Mfuko pamoja na Kamati ya Kuchochea Maendeleo ya Jimbo ili kuweza kutekeleza kwa ufanisi sheria hiyo. Tarehe 5 Februari, 2010 kanuni ya kuweka utaratibu wa kusimamia na kuratibu miradi ya maendeleo itakayoanzishwa katika majimbo ziliandaliwa.

Mheshimiwa Spika, kufuatia hoja ya marekebisho ya sheria Serikali iko tayari kuanisha maeneo au vifungu vya sheria ambavyo vinachangamoto katika utekelezaji wa Sheria ya Mfuko

wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo ili viweze kufanyiwa kazi pamoja na maoni mengine yatakayotolewa na wadau kuhusu sheria hiyo.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kassim Haji.

**MHE. KASSIM HASSAN HAJI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana na ninamshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake, lakini ninaomba nimuulize.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa sheria hizi za manunuzi za Mfuko wa Jimbo wa Tanzania bara na Zanzibar zinakinzana na kwa kuwa Wabunge wengi wa Zanzibar wanaingiziwa pesa hizo katika halmashauri; je, ni lini sasa Serikali itakuja na muswada huo hapa ili kurebisha kuondoa shida ambayo ipo kwa muda mrefu? Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF):** Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge Kassim kama alivyoliuliza na nimpongeze kwa kuleta hoja hii na swali hili.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI tumeendelea kupokea maoni ya wadau mbalimbali, Kamati za Bunge, lakini pamoja na baadhi ya Wabunge ambao wametuletea maoni Ofisi wa Waziri Mkuu, TAMISEMI kuhusiana na sheria hii na namna ya kuratibu mfuko huu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nimhakikishe Mheshimiwa Kassim pamoja na Wabunge wengine kwamba Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI inaendelea kuliratibu hili na kupokea maoni ili kuweza sasa kuelekea kwenye kufanya mabadiliko na kuboresha namna ya kuweza kuutoa mfuko huu na kuhudumia wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Mheshimiwa *Engineer* Fadhili.

**MHE. ENG. FADHILI S. CHILOMBE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwanza ninaishukuru na kuipongeza Serikali kwa uamuzi wake wa kutoa mfuko huu kwa ajili ya maendeleo ya majimboni kwetu.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa ninaomba kujua kwamba kwa kuwa wakati wa uamuzi huu ulipokuwa unafanyika ni tofauti na sasa, kwamba hali ya maisha imepanda na gharama za vitu zimeongezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali haioni haja sasa ya kuongeza kiwango cha fedha inayopelekwa majimboni ili kutuwezesha kupambana hali tuliyonayo? *(Makofi)*

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Najma Murtaza Giga) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Fadhili kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI kama nilivyosema awali tunaendelea kupokea maoni na haya ni maoni ambayo Mheshimiwa Fadhili ameyatoa na Wabunge wengi humu ndani wameendelea kutoa maoni hayo na sisi tupo tayari kuendelea kuyafanyia kazi maoni hayo na pindi itakapokuwa tayari, Serikali itakuja mbele ya Waheshimiwa Wabunge kuwaambia nini tumefanya na nini kimeongezeka ili kuweza kuboresha mfuko huu na ukalete tija kwenye majimbo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Mhe. Dkt. Christina Mnzava.

**MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, kwa kuwa Serikali imesema italeta marekebisho ya sheria ya kuhusu Mfuko wa Jimbo na tunajua kabisa kwamba Wabunge wote humu ndani tunahaki sawa na tunafanya kazi kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, haioni kwamba katika kurekebisha sheria hizo ikawa-*include* Wabunge wa Viti Maalum kwenye Mfuko wa Jimbo kwa sababu na wenyewe wanafanyakazi kwa wananchi? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Christina Mnzava, Mbunge wa Mkoa wa Shinyanga kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema awali tayari Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI tumeanza kuratibu kwa kupokea maoni haya na nichukue kama maoni maana yake ni swali dogo lakini nichukue kama maoni kwamba tuwa-*accommodate* kwenye namna ya kwenda kufanyia mabadiliko ili sasa kuona namna gani mfuko huu tutaweza kuutanua na ili Wabunge waweze kuwa na nguvu kule majimboni kuweza kupitia miradi ambayo imekwama waweze kuikwamua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na swali la Mheshimiwa Hamoud Abuu Jumaa, Mbunge wa Kibaha Vijijini; kwa niaba Mheshimiwa Hawa Chakoma.

Na. 519

**Ujenzi wa Barabara ya Kongowe – Soga**

**MHE. HAWA M. CHAKOMA K.n.y. MHE. HAMOUD A. JUMAA** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Barabara ya Kongowe - Soga kwenye *station* ya Soga kwa kiwango cha lami?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Hamoud Abuu Jumaa, Mbunge wa Jimbo la Kibaha Vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua umuhimu wa ujenzi wa Barabara ya Kongowe – Soga yenye urefu wa jumla kilometa 17.5, kwani itarahisisha usafiri na usafirishaji kwa wananchi watakaotumia huduma za treni, kupunguza msongamano wa magari, pamoja na kuboresha barabara zinazohudumia shughuli za viwanda ambapo kwa sasa imeanza kufanyiwa usanifu wa kina kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mara baada ya usanifu kukamilika na gharama halisi za utekelezaji kufahamika, Serikali itatenga fedha kwa ajili ya ujenzi, lakini katika mwaka wa fedha 2023/2024, shilingi milioni 500 zilitumika kuboresha Barabara ya Kongowe–Soga jumla ya kilometa nane kwa kiwango cha changarawe. Kazi zilizotekelezwa zilijumuisha ujenzi wa makalavati, uchimbaji na ujenzi wa mitaro ya maji, pamoja na kuziba mashimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka wa fedha 2025/2026 jumla ya shilingi milioni 44.2 zimetengwa kwa ajili ya kufanya matengenezo ya Barabara ya Kongowe – Soga kilometa nane.

Aidha, Serikali imeweka katika mpango wa mwaka 2026/2027 ujenzi wa sehemu korofi kwa gharama ya shilingi milioni 279.9

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kuihudumia barabara hii kwa matengenezo, ujenzi na ukarabati kulingana na upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hawa Chakoma.

**MHE. HAWA M. CHAKOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali na naomba niulize maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Waziri pamoja na majibu mazuri ya Serikali ninachotaka kufahamu, kwa kuwa barabara hiyo iko katika hatua ya usanifu kama ambavyo umesema na kwa kuwa barabara hiyo ni muhimu sana kwa namna vile ulivyosema inatuunganisha na stesheni ya *SGR,* lakini pia kuna Kiwanda kikubwa cha Nyama cha *Tanchoice* ambacho kinafanya biashara kubwa sana kule na kwa kuwa barabara ile haipitiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni upi mpango wa muda mfupi wa Serikali ili kuhakikisha huduma inaendelea kupatikana kama ilivyokuwa awali?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili, kwa kuwa umesema barabara ile ina kilometa 16.5 tu, ni kwa nini sasa barabara hii isitoke kwa *TARURA* na ikaenda kwa *TANROADS* kwa umuhimu wa barabara hii? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu maswali madogo ya nyongeza ya Mheshimiwa Hawa kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango wa Serikali mfupi wa kuhakikisha barabara hii tuna ihudumia na tunairudisha katika hali yake, kwa kutumia Bunge lako Tukufu hili nimuelekeze Meneja wa *TARURA* Wilaya afike katika maeneo ambayo Mheshimiwa Mbunge ameyaainisha kufanya tathmini na kutuletea andiko Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI na kuona namna gani tutachukua hatua za dharura ili kuweza kufanikisha miundombinu hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili ni jibu kwa ujumla, mtaona kwamba kuanzia mwaka 2020 mpaka 2021, bajeti yetu ya *TARURA* ilikuwa wastani wa shilingi bilioni 275 lakini mpaka leo hii, mwaka 2026/2027 tumetenga zaidi ya shilingi bilioni 871 ambalo ni ongezeko la zaidi ya mara tatu ya kile ambacho tulikuwa tukikitekeleza mwaka 2021.

Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge pamoja na Wabunge wengine kwamba tunaenda kuongeza nguvu katika *TARURA* na kuweza kuzihudumia barabara zetu hizi, ninaomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Subira Mgalu, na Mheshimiwa Hawa Mwaifunga ajiandae.

**MHE. SUBIRA K. MGALU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, kwa kuwa Serikali mwaka 2025 kupitia Waziri wa TAMISEMI, iliahidi kutoa kiasi cha shilingi bilioni moja kwa ajili ya ujenzi wa barabara kwenye Kata ya Kerege, kuelekea eneo la viwanda, ambako moja ya kiwanda kilichopo ni cha kuunganisha magari, kiwanda cha pekee Afrika Mashariki ya Kati. Je, ni lini Serikali itatimiza ahadi hii kwa ajili ya Kata ya Kerege? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, ninaomba kujibu swali la nyongeza kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge ameliuliza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba ahadi za Serikali tutazitimiza kwa kadri

ambavyo tunavyopokea bajeti. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwa maeneo ya barabara ambayo ameyaainisha, tutaendelea kutenga fedha ili kutekeleza ahadi hizo ili kuendelea kutoa huduma ambayo Serikali imekusudia katika maeneo hayo, ninaomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hawa Mwaifunga, ajiandae Mheshimiwa Jonas Mbunda.

**MHE. HAWA S. MWAIFUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kuniona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kata ya Mbugani, barabara nyingi hazipitiki na ni mbovu, zina mashimo mengi. Barabara ya Kamna – Tandale – Sekulu - Mzaganza – Usule - Miembemingi na Tandale mpaka Kiwanda cha Nyuzi; barabara hizi zina hali mbaya na mvua ziliponyesha kuna mashimo makubwa kiasi kwamba wananchi wanashindwa kufanya shughuli zao kwa sababu ya ubovu wa barabara.

Nini kauli ya Serikali juu ya kufanya ukarabati wa barabara hizi, angalau mtujengee kwa kiwango cha changarawe ili wananchi hawa wa Kata ya Mbugani waweze kupata tabasamu?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Hawa Mwaifunga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa swali ambalo ameliuliza na mimi huwa ninapita njia ile ya Tabora, kwa hiyo, huwa nyingi huwa zinaathiri sana ule mji wetu wa Tabora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumhakikisha tu Mheshimiwa Hawa Mwaifunga, sasa mvua zile za masika zinaelekea ukingoni

na bajeti ya *TARURA* imeongezeka maradufu, ukiangalia kutoka mwaka 2021 mpaka leo imeongezeka zaidi ya mara tatu.

Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Hawa Mwaifunga, tutatenga bajeti kwa ajili ya kurekebisha barabara hizi kwa kiwango cha changarawe ili ziendelee kutoa huduma katika jimbo lake na wananchi waendelee ku-*enjoy* tabasamu la Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Ninaomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jonas Mbunda.

**MHE. JONAS W. MBUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Barabara ya Mbinga - Mbangamao hadi Mpepai kilometa 32 imeharibiwa sana na mvua katika kipindi kirefu. Ni lini Serikali itafanya mkakati wa kuhakikisha kwamba barabara hiyo inatengenezwa?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu swali la nyingeza la Mheshimiwa Mbunge kama ambavyo ameliuliza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI tulifanya tathmini ya barabara zote nchini na hadi kufukia barabara zote za wilaya ambazo zinahudumiwa na *TARURA* mpaka sasa tuna jumla ya kilometa 47,000 na zaidi ya kilometa 47,000 ambayo ni sawasawa na zaidi ya 32.9% ambazo zina hali mbaya nchini na barabara hizi zinahitaji jumla ya shilingi bilioni 264 kufanyiwa marekebisho zirudi katika hali yake.

Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwa sababu tunaelekea mwisho wa msimu wa mvua tutatenga bajeti kwa ajili ya matengenezo ya barabara hizo ili ziendelee kupitika na kutoa huduma kwa wananchi, ninaomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zuberi Mfaume, swali la nyongeza

**MHE. ZUBERI Y. MFAUME:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa ya kuuliza swali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Barabara ya Kata ya Bwakira Juu inayounganisha na Kata ya Bwakira Chini, barabara hii sasa haipitiki, sio tu kwa gari, hata kwa pikipiki. Je, ni lini sasa Serikali itafanya ukarabati wa barabara hii ili iweze kupitika?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Zuberi Mfaume, kama alivyoliuliza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyojibu kwenye majibu yangu ya awali, Mkoa wa Morogoro unafahamika kijiografia unapokea maji mengi sana kutoka mikoa mingine kutoka Manyara, kwa hiyo, zile barabara zinaharibika hata kama mvua hazinyeshi katika Mkoa wa Morogoro.

Kwa hiyo, nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge, pamoja na wananchi ambao wanawahudumia, *TARURA* tutaendelea kutengea bajeti ili kurekebisha barabara hizi, ninaomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwita Getere.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru, sijajua sasa kitu gani kinatokea katika Wilaya, Jimbo la Bunda; wakandarasi wote wamesimama kwa sababu hawana fedha. Sasa ni lini mtawalipa wakandarasi wa Bunda ili waendelee na barabara zao?

**MWENYEKITI:** Umemwelewa Mheshimiwa Waziri? Majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Getere, kama alivyoliuliza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekwishafanya tathmini katika wilaya zote nchini na tumekwishaandaa mpango, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, kama nilivyosema zaidi ya bilioni 264 zinatakiwa ili ziende kwa wakandarasi wetu waweze kutengeneza barabara hizi.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Getere nikuhakikishie, tutakapotenga bajeti Serikali tutakupa taarifa ili tuhakikishe kwamba unakwenda kuzisimamia fedha hizi kwa wakandarasi hawa ili wazijenge barabara hizi kwa kiwango kinachotakiwa, ninaomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na swali la Mheshimiwa Bakari, Bakari Shingo, Mbunge wa Ukonga, aulize swali lake.

Na. 520

**Ujenzi wa Barabara ya Pugu – Mnadani – Bangulo hadi Ulongoni B**

**MHE. BAKARI B. SHINGO** aliuliza:-

Je, lini ujenzi wa Barabara ya Pugu – Mnadani – Bangulo hadi Ulongoni B utaanza?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Bakari Bakari Shingo, Mbunge wa Jimbo la Ukonga kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Barabara ya Pugu – Mnadani – Bangulo hadi Ulongoni B ina urefu wa jumla ya kilometa 4.36 ambapo imetengewa jumla ya shilingi bilioni 2.017 kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami urefu wa kilometa 1.2.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa ujenzi huu unafanyika kwa awamu mbili; awamu ya kwanza ni urefu wa

kilometa 0.3 kwa gharama ya shilingi milioni 575.526 kupitia chanzo cha mapato ya ndani ya halmashauri na ujenzi wa awamu ya pili una urefu wa kilometa 0.9 kwa gharama ya shilingi bilioni 1.442 kupitia fedha za jimbo na tozo za mafuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa awamu ya kwanza umekamilika, kwa sasa mkandarasi anaendelea na Ujenzi wa awamu ya pili, ambapo utekelezaji wake umefikia 10%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kuhudumia mtandao wa barabara wa Jimbo la Ukonga kwa kujenga, kufanya ukarabati na Matengenezo kulingana na upatikanaji wa fedha, ninaomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bakari Shingo.

**MHE. BAKARI B. SHINGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, ninapenda nimjulishe tu kwamba, hii 0.3% kipande cha Mwembe Subu kuelekea Mwembe Kiboko, mkandarasi aliyekuwepo pale kwa awamu ya kwanza hadi tunavyozungumza leo bado miferiji haijajengwa, lakini pia hiyo 10% unayoizungumza kutoka Mwembe Subu kwenda Mwembe Kiboko, Mheshimiwa Waziri nimjulishe tu kwamba mkandarasi alifika kama ku-*survey* na alivyoondoka hajarudi tena. Kwa hiyo sijui hata 10% iko imepimwa kwa kiwango gani ama kwa kuanzia wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo tu, nilitaka nijue tu, Mheshimiwa Waziri anatuambia nini kuhusu barabara ambazo nyingi zimeharibika kipindi hiki cha mvua na hazipitiki, ikiwa ni pamoja na Barabara za Zingiziwa, Barabara za Buyuni, na Chanika. Nyingi sana, imekuwa ni aibu sana, sehemu zingine tumeshuhudia akina mama ili wapite inabidi iwe kama wanavua nguo, kitu ambacho ni kinyume na ustaarabu wetu. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF):** Mheshimiwa

Mwenyekiti, naomba kujibu maswali madogo ya nyongeza ya Mheshimiwa Bakari Shingo, Mbunge wa Jimbo la Ukonga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema awali, tayari tathmini tumeshafanya katika majimbo yote na wilaya zote nchini na kuandaa bajeti ambayo itakwenda kujenga barabara hizi ambazo Mheshimiwa Mbunge ameziainisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwondoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge na kupitia Bunge lako Tukufu, nimwelekeze Meneja wa *TARURA* Kanda ya Dar es salaam aweze kuwasilisha tathmini na afike katika maeneo ambayo Mheshimiwa Mbunge ameyaainisha hapa ili kuona namna gani ya kuweza kuanza na kuendelea kuratibu na ufuatiliaji wa karibu wa barabara hizi ambazo Mheshimiwa Mbunge ameziainisha, ninaomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Exaud Kigahe, Mheshimiwa Haidary Sumry ajiandae.

**MHE. EXAUD S. KIGAHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Jimbo la Mufindi Kaskazini na hasa kata tatu; Kata ya Ifwagi, Mdabulo na Ihanu ni kata ambazo ziko ukanda wa juu kwenye mvua nyingi sana. Barabara kutoka Mkuta kwenda Ludilo - Irasa mpaka Ihanu imeharibika sana zaidi ya miaka mitatu sasa haijakarabatiwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu alipokuja kwenye jimbo langu pale Ifwagi, wananchi walileta malalamiko kuna wananchi hasa akina mama wanaojifungua, wanapoenda hospitali wanajifungulia njiani na wengine wanakufa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lini sasa Serikali itakarabati barabara hii kutoka Mkuta – Ludilo – Ihanu - Mdabulo mpaka Irasa ili wananchi hawa waweze kusafiri kwenda kupata huduma za afya na mambo mengine?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge kama alivyoliuliza kuhusiana na Jimbo la Mufindi Kaskazini kwa changamoto ya barabara ambazo ni mvua nyingi ambazo nchi yetu ilipokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kwa bajeti ambayo tumeitenga, *TARURA* itaendelea kwenda kurekebisha barabara zile ambazo Mheshimiwa Mbunge ameziainisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo ambalo la faraja ni lile ambalo kamati zetu zilishauri, lakini pia Mheshimiwa Waziri Mkuu alitoa maelekezo kwamba zile fedha za tozo ziende moja kwa moja kwenye Mfuko wa *TARURA* ili waweze kuzirekebisha barabara hizi kwa wakati.

Nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge pamoja na Wabunge wengine, tutaendelea kuelekeza fedha katika maeneo hayo ili kwenda kukamilisha miundombinu hiyo, ninaomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Haidary Sumry.

**MHE. HAIDARY H. SUMRY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, Jimbo la Mpanda Mjini, Barabara ya Mlimani *City* kutoka Kata ya Nsemulwa kwenda Kata ya Uwanja wa Ndege, barabara hii ilitangazwa na akapatikana mkandarasi, lakini mpaka sasa hivi huyo mkandarasi hajaruhusiwa kufanya ile kazi na kuna daraja pale ambalo linaunganisha hizi kata mbili, wazazi ambao wanatakiwa kutoka kwenye Kata ya Uwanja wa Ndege kuja Kata ya Nsemulwa wanashindwa kupita kutokana na daraja hilo kutokamilika.

Ni nini kauli ya Serikali kuhusu mkandarasi kumruhusu ili aweze kuanza kazi ya ujenzi wa barabara hii?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. JAFAR R. SEIF):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge wa Mpanda Mjini kama alivyoliuliza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza tutambue, mpango wa Serikali ulikuwa ni kulipa madeni ya nyuma ya wakandarasi wote ili tunapoenda kuanza kutekeleza bajeti hii tusiwe na madeni mengi ya nyuma.

Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, Serikali imekwishalipa madeni mengi ya wakandarasi wa nyuma na fedha hizi ambazo tunakwenda kutekeleza bajeti ya mwaka 2026/2027 itakwenda moja kwa moja kwenye maeneo ambayo Serikali imeelekeza na hatutakuwa na madeni makubwa ya nyuma. Hivyo Mheshimiwa Mbunge nikuhakikishie na wananchi wa Mpanda Mjini kuwa tutaelekeza fedha katika daraja hilo na kumlipa mkandarasi ili aanze kazi. Kwa hiyo, ninaomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu hayo ya Waheshimiwa Wabunge kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI.

Tunaendelea sasa na Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Isaya Moses Mngurumi, Mbunge wa Kongwa aulize swali lake.

Na. 521

**Uchimbaji wa Bwawa la Chilanilizi – Ngomai**

**MHE. ISAYA M. MOSES** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuanza uchimbaji wa Bwawa la Chilanilizi, Kata ya Ngomai – Kongwa?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Uchukuzi kwa niaba ya Waziri wa Kilimo.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI K.n.y. WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Isaya Mngurumi Moses, Mbunge wa Kongwa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji ilitenga fedha katika bajeti ya mwaka wa fedha 2025/2026 kwa ajili ya ujenzi wa Bwawa la Maji Chilanjilizi, Kata ya Ngomai ambapo upembuzi yakinifu wa mradi huu umekamilika kwa 100%. Kwa sasa Tume imeingia mkataba wenye thamani ya shilingi bilioni 106 kwa ajili ya kuanza utekelezaji wa mradi wa uchimbaji na ujenzi wa bwawa hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kukamilika kwa Mradi wa Bwawa la Chilanjilizi unatarajiwa kunufaisha vijiji vinavyozunguka eneo la mradi ikiwemo Chilanjilizi, Manyaya, Sigoni na Ngomai na maeneo mengine yanayozunguka mradi huo na hivyo kutoa fursa kwa wananchi kupata fursa ya uhakika wa maji kwa ajili ya kilimo na shughuli nyingine za kiuchumi na kijamii.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Isaya Mngurumi.

**MHE. ISAYA M. MOSES:** Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa huu mradi utawainua sana wananchi wa Kongwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabla ya kusema hivyo nishukuru sana kwa majibu mazuri ya Serikali yanatupa matumaini makubwa, kwa utekelezaji wa huu mradi, maana yake ni kwamba wananchi wangu wa Vijiji vya Kata za Ngomai, Kata ya Ngomai, Mtanana, Songambele, Mkoka pamoja na Matongolo, Makawa pamoja na Njoge watanufaika zaidi katika huu mradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu, ni lini sasa utekelezaji wake utaanza kwa sababu tayari sasa watu walishapisha huu mradi, lakini umechukua muda mrefu, sasa familia zimeanza kurudi katika haya maeneo. Wanasema kwamba mradi hautakuwepo, tusipoangalia itatuingiza tatizo la kulipa fidia sasa tuone tutajipangaje katika eneo hili?

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, Kongwa sio mbali, nimuombe Mheshimiwa Waziri akipata nafasi twende

tukatembelee pale, tukaone hali halisi na tukatembelee watu wana shida ya maji kule, twende tukakutane nao. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu. Mheshimiwa Waziri jibu la kwanza, la pili ninafikiri ni la mwenyewe Waziri wa Kilimo.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI K.n.y. WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa ya kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Isaya Mngurumi Moses nikiwa najibu kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kwanza tunampongeza Mheshimiwa Mbunge kwa jinsi ambavyo ameanza kazi vizuri, anafuatilia maslahi ya wananchi wa Kongwa na kwa kweli kwa kutambua umuhimu wa mradi huu ndiyo maana Serikali kwanza ilitambua, pili ikafanya usanifu na tatu, baada ya kutazama na kutambua gharama zote, ikaamua kusaini mkataba wa zaidi ya shilingi bilioni 106 ili kazi ianze.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba hii ni moja ya miradi ambayo inatarajiwa kuanza kutekelezwa katika mwaka wa fedha ujao. Kwa hiyo, nimwombe awe na subira ili Serikali ikaweze kufanya mradi huu muhimu kwa wananchi wa jimbo zima la Kongwa na hili la pili, naamini Waziri wa Kilimo amesikia au Naibu Waziri, wakati ukifika watakwenda naye kwa ajili ya kuhakikisha kwamba wanatazama kulingana na maombi ya Mheshimiwa Mbunge.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri Wizara ya Uchukuzi kwa kujibu maswali hayo ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo.

Tunaendelea na Wizara ya Maji, Mheshimiwa Sikudhani Yasin Chikambo, Mbunge wa Viti Maalum, aulize swali lake.

Na. 522

**Kusimama kwa Mradi wa Maji – Tunduru**

**MHE. SIKUDHANI Y. CHIKAMBO** aliuliza:-

Je, lini Serikali itamlipa mkandarasi ili kukamilisha Mradi wa Maji Tunduru ambao umesimama?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Sikudhani Yassini Chikambo, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inaendelea na utekelezaji wa mradi wa maji unaolenga kunufaisha Mji wa Tunduru unaogharimu zaidi ya shilingi bilioni 3.4. Mradi huo upo kwenye hatua za awali za utekelezaji ambapo unahusisha ujenzi wa dakio, ujenzi wa tenki lenye ujazo wa lita 1,000,000 sanjari na ulazaji wa mabomba umbali wa kilometa 98.7.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali tayari imepeleka jumla ya shilingi 511,327,133.14 ikiwa ni fedha za malipo ya awali kwa maana ya *advance payment* kwa mkandarasi na wazabuni wanaohusika katika utekelezaji wa mradi huo. Hivyo, ninamwelekeza Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Tunduru kuharakisha uratibu wa malipo kwa wahusika ndani ya siku saba kuanzia leo.

Aidha, nimtake mkandarasi kurejea eneo la kazi ili kuendelea na utekelezaji wa mradi huo unaolenga kunufaisha zaidi ya wananchi 75,674 wa Mji wa Tunduru na viunga vyake, ninakushukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sikudhani Chikambo.

**MHE. SIKUDHANI Y. CHIKAMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, ni kweli kama alivyosema Naibu Waziri kwamba mradi ule unatekelezwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru na kwa hakika wananchi karibia 75,000 watanufaika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipende kwanza kuishukuru Serikali kwamba kwa pesa hizi ambazo wamepeleka shilingi milioni 500

ninashukuru sana zitamwezesha mkandarasi kurudi *site,* lakini nilitamani kujua, kwa kuwa mradi huu ulitakiwa ukamilike mwezi wa tano mwaka huu, ni lini sasa kiasi cha pesa kilichobaki kitapelekwa ili kukamilisha huu mradi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili, pamoja na mradi huu ambao unatekelezwa katika viunga vya Tunduru Mjini, lakini uko mradi mwingine upo katika Kata ya Namwinyu, mradi ule ulitakiwa ukamilike mwaka jana mwezi wa saba. Wanufaika wa mradi ule ni vijiji viwili vya vya Namwinyu na Namakungwa. Kiasi cha pesa kilichobaki ni shilingi milioni 120. Nilitamani kujua na ule mradi utakamilika lini ili wananchi wetu waendelee kunufaika? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Sikudhani Yassini Chikambo, Mbunge wa Viti Maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge kwa kuendelea kufuatilia kwa ukaribu miradi inayotekelezwa ndani ya Halmashauri ya Tunduru, lakini pia niendelee kumuomba Mheshimiwa Mbunge kuendelea kufuatilia ili na sisi tunapopata jicho la pili katika utekelezaji wa miradi inatusaidia sana kujua mienendo ya wakandarasi ambao tunawapatia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimtoe hofu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan katika huu Mji wa Tunduru ambao una majimbo mawili, tunafahamu pale kuna Mheshimiwa Ado Shaibu, lakini pia kuna Mheshimiwa *Engineer* Fadhili, ambapo ndani ya kipindi cha Bunge hili linaloendelea Mheshimiwa Rais ameshapeleka fedha, kwanza kabisa tulipeleka shilingi milioni 200, lakini sasa tumepeleka shilingi milioni 500, maana yake kwamba inaonesha dhahiri kabisa kwamba Mheshimiwa Rais amedhamiria kuhakikisha kwamba miradi hii inakamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimtoe hofu, mradi huu utakamilika, lakini pia tunatambua inawezekana ikawa nje ya

muda ambao tulikuwa tumekusudia hapo mwanzoni, lakini nikutoe hofu, tutaongeza nguvu na tutamsimamia mkandarasi kwa ukaribu zaidi ili ahakikisha kwamba anakamilisha na maji yanatoka ili Watanzania wapate huduma hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hili eneo la pili, nikutoe hofu pia kwamba huo mkakati wetu wa kuendelea kutatua changamoto za miradi inayoendelea si kwamba itawezekana miradi yote tukaikamilisha kwa pamoja, tutaenda awamu kwa awamu, lakini kama ambavyo nimesema katika majibu yangu ya msingi fedha hizi zimeshapelekwa. Pia tutaweka utaratibu mwingine wa kwenda kupeleka fedha katika eneo ambalo Mheshimiwa Mbunge ameliomba. Ninakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Emmanuel Khambay, na Mheshimiwa Amina Mkumba ajiandae.

**MHE. EMMANUEL J. KHAMBAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Halmashauri ya Mji wa Babati kuna mradi wa mabwawa manne ya majitaka. Tunaishukuru Serikali kwa kulipa fedha kwa *certificate* ya kwanza; *certificate* ya pili inahitaji shilingi bilioni 2.6 na tunaishukuru Serikali juzi kwa kutuwekea shilingi milioni 700.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lini Serikali itamalizia shilingi bilioni 1.9 ili mkandarasi aliyeondoka *site* aweze kurudi na kuweza kutatua changamoto au ukamilishaji wa mabwawa hayo ili wananchi waendelee kunufaika na huduma hiyo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI**: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Emmanuel kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa, kwanza nimpongeze kwa kuendelea kuwapigania wananchi wake na kwa kufuatilia malipo ya wakandarasi. Pia tunatambua kwamba wakandarasi tunapowalipa hata ile fedha ndogo ukiwalipa

wanashindwa kurudi *site* kwa sababu unakuta kwamba wame-*engage* na miradi mingi sana. Siyo miradi pekee yake ya maji, wanakuwa wame-*engage* na miradi mingine; *TARURA*, umeme, na kadhalika, kiasi kwamba ukimlipa ile fedha mara nyingine inaenda kulipwa benki na matokeo yake anashindwa kurudi *site*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tumeanzisha utaratibu mwingine tofauti wa kuhakikisha kwamba kabla hatujamlipa mkandarasi tunawaita na kukubaliana ili kuhakikisha kwamba ile *security* yake iweze kuwa *specific* kwa ajili ya mradi husika na pesa inapolipwa basi iende kutekeleza mradi husika.

Kwa hiyo, nimtoe hofu hii shilingi bilioni 1.9 ambayo imebaki pamoja na kumlipa shilingi milioni 700 hajarudi, tutamlipa hii shilingi bilioni 1.9 kuunganisha na ile ili ifikie ile *certificate* ya shilingi bilioni 2.6 aweze kurudi *site* na kuendelea na mradi ili Watanzania wapate huduma ya maji safi na salama. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Amina Mkumba, ajiandae Mheshimiwa Isack Copriano na Mheshimiwa Charles Njama.

**MHE. AMINA M. MKUMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kuniona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lini Serikali itakamilisha mradi wa uchimbaji wa visima 10 katika Kata ya Kibiti, Jimbo la Kibiti ili wananchi waweze kupata maji safi na salama? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI**: Mheshimiwa Mwenyekiti, uchimbaji wa visima 10 katika Jimbo la Kibiti ulikuwa ni mkakati wa Serikali kuchukua hatua za dharura ili kutatua changamoto ya upatikanaji wa maji safi na salama, na ninamshukuru sana Mheshimiwa Mbunge kwa kuendelea kukumbushia hili, na sisi lipo ndani ya vipaumbele vyetu ili kuhakikisha kwamba tunapeleka fedha zaidi na wakandarasi waweze kuhakikisha kwamba mradi huu unakamilia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafahamu miradi ambayo tunayo inayoendelea nchi nzima zaidi ya 1,206 ni mingi, lakini tutaendelea kuhakikisha kwamba tunatoa vipaumbele kwenye miradi ambayo ni ya kimkakati na ambayo ikitoa matokeo basi inaweza kuwa imetatua changamoto kubwa kwa wananchi. Nimtoe hofu Mheshimiwa Mbunge eneo lake tutalipata kipaumbele kwa ajili ya utekelezaji. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Isack Copriano.

**MHE. ISACK J. COPRIANO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi nichukue nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri anajua fika kwamba kuna miradi Monduli ambayo inaendelea na kimsingi hali ya Monduli ya maji siyo nzuri.

Je, huoni sasa ni wakati muafaka mitambo ile ambayo Mheshimiwa Rais alinunua kwenye Kanda yetu ya Kaskazini ikaenda kuchimba baadhi ya maeneo kama Esilalei, Moita na Nagharami kuchimba mabwawa ili angalau basi iweze kuwasaidia wananchi pale wakisubiri maji yale ya vijiji 13 na vijiji saba yafike?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI**: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Isack Copriano, Mbunge wa Monduli kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge kwa kuendelea kufuatilia utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ndani ya jimbo lake na pia kwa kuendelea kutupatia ushirikiano pale ambapo tunatoa taarifa za wakandarasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimtoe hofu, mitambo hii Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan aliinunua kwa ajili ya Watanzania na sauti ya Mbunge ni sauti ya Watanzania. Sisi

tunapokea na tutahakikisha kwamba mitambo hii itaenda kutumika kwa maslahi ya Watanzania hasa katika maeneo ya Monduli ambayo Mheshimiwa Mbunge ameomba, lengo kuu ni kuhakikisha kwamba upatikanaji wa maji yenye uhakika uweze kutokea katika Jimbo la Munduli. Nakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Charles Njama.

**MHE. CHARLES M. NJAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Jimbo la Korogwe Mjini wameahidiwa kupata maji kutoka katika Mradi wa Maji wa Miji 28, karibia ahadi tatu tofauti tofauti. Tuliahidiwa kupata maji mwezi wa tatu, baadaye tukaambiwa mwezi wa tano na mpaka sasa bado maji hayajaanza kutoka katika mradi ule wa miji 28.

Je, ni lini wananchi wa Mji wa Korogwe Mjini wataanza kupata maji kutoka katika Mradi wa Miji 28 wa Mwanga – Same - Korogwe? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI**: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ile *package* kwanza kabisa hatuna changamoto ya kifedha na pili mradi huu unaendelea vizuri kabisa na usimamizi wake uko vizuri kabisa. Tunatambua kwamba tulikuwa na matumaini ya kuukamilisha mapema, lakini miradi hii ni *design and building.* Sasa unapo-*design* na ku-*build* mara nyingine kunakuwa na kubadilika badilika kwa utaratibu wa namna ya kuutekeleza mradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunafahamu kwamba tulikuwa tumeahidi mwezi wa tatu, lakini, haijatokea hivyo ni kwa sababu ya *model* ambayo tulichagua katika utekelezaji wa mradi huo. Nimtoe hofu mradi huu unaendelea vizuri kabisa na tunaamini kwamba bado tuko ndani ya muda wa mkataba ambao mkandarasi alikuwa amepatiwa.

Kwa hiyo, nimtoe hofu mradi huo tutaendelea kuusimamia kwa ukaribu ili uweze kutoa matokeo yaliyokusudiwa kwa wananchi wa Korogwe. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Tunakushukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu hayo kwa Waheshimiwa Wabunge kutoka Wizara ya Maji.

Tunaendelea sasa ni Wizara ya Ujenzi, Mheshimiwa George Natany Malima, Mbunge wa Mpwapwa, aulize swali lake.

Na. 523

**Ujenzi wa Daraja la Godegode**

**MHE. GEORGE N. MALIMA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Daraja la Godegode kwa kuwa mkandarasi ameshapatikana?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA UJENZI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa George Natany Malima, Mbunge wa Mpwapwa, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, taratibu za manunuzi ya kumpata mkandarasi wa ujenzi wa Daraja la Godegode zimekamilika. Kwa sasa tunaendelea kutafuta fedha za malipo ya awali *(advance payment)* ili mkataba usainiwe na kazi ya ujenzi ianze, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa George Malima.

**MHE. GEORGE N. MALIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini, nina maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza, kwa kuwa mkandarasi alipatikana muda mrefu sasa, lakini ujenzi haujaanza, wananchi wa Godegode na

maeneo yanayozunguka wanaomba kujua nini tamko la Serikali na lini malipo ya awali yatatolewa kwa mkandarasi ili ujenzi uanze ili wananchi waendelee kufanya shughuli zao za kiuchumi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, daraja hili linaunganisha majimbo mawili; Jimbo la Kibakwe na Jimbo la Mpwapwa na wananchi wa maeneo yote mawili shughuli zao za kiuchumi zimesimama kwa sababu ya kukatika kwa mawasiliano ya barabara.

Je, kwa nini Serikali haioni umuhimu wa kujenga daraja la muda ili wananchi hawa wakati wanasubiri taratibu za Serikali zikiendelea waendelee kufanya shughuli zao za kiuchumi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa George Natany Malima, Mbunge wa Jimbo la Mpwapwa, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza kuhusu ni lini? Ni kweli mradi huu umesisitizwa sana na ni maelekezo ya viongozi wetu, Mheshimiwa Waziri Mkuu hapa karibuni alipofanya ziara alitoa maelekezo haya na nimshukuru sana Mheshimiwa George Natany Malima kwa msisitizo wa kutukumbusha katika kuhakikisha kwamba wananchi wa hapa Mpwapwa na Kibakwe na uzuri daraja hili pia siyo tu Mpwapwa na Kibakwe, linaunganisha na Mkoa wa Morogoro, Wilaya ya Kilosa. Kwa hiyo, ni daraja muhimu sana na ni kiungo cha wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimtoe hofu, tumeliweka katika *priority* kwamba zile mita 154 zote zimeshapata mkandarasi, fedha ya *advance* itakayokuja wakati wowote sasa tutamlipa mkandarasi yule katika kumtia msisitizo wa maelekezo ya viongozi wetu, Mheshimiwa Waziri Mkuu juzi alipofanya ziara katika Mkoa huu wa Dodoma.

Kwa hiyo, nimtoe hofu Mheshimiwa George Natany Malima na Wana-Mpwapwa, Kibakwe na hata Wilaya ya Kilosa kwamba mradi huu tunakwenda kuufanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan hapa mkoani Dodoma imeondosha hizi *bottleneck* nyingi ikiwa ni pamoja na kujenga madaraja tisa ya namna hii. Katika barabara kuu ya Morogoro kuja Dodoma tumejenga madaraja manne na barabara ya kutoka Dodoma kwenda Iringa tumejenga madaraja matatu na pale Chamwino Daraja la Nzali tumelikamilisha pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jumla ya shilingi bilioni 33.3 zimetumika. Kwa hiyo, ninataka niwahakikishie Wana-Dodoma, Wana-Kibakwe, Wana-Mpwapwa na Wana-Kilosa na Watanzania kwa ujumla, tutalipa jambo hili kipaumbele na nimpongeze sana Mheshimiwa George Natany Malima kwa kulipigania jambo hili kwa uzalendo mkubwa sana. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na swali la Mheshimiwa Husna Juma Sekiboko, Mbunge wa Viti Maalum.

Na. 524

**Ujenzi wa Barabara ya Lushoto – *Umba Junction***

**MHE. HUSNA J. SEKIBOKO** aliuliza: -

Je, lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Barabara ya Lushoto, Magamba, Lukozi, Mlalo mpaka *Umba Junction* kwa kiwango cha lami?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA UJENZI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Husna Juma Sekiboko, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Barabara ya Lushoto – Magamba – Lukozi – Mlalo hadi *Umba Junction* kilometa 66.35, ni barabara inayohudumiwa na Wakala ya Barabara Tanzania *(TANROADS)*, Mkoa wa Tanga. Kwa sasa Serikali inaendelea na maandalizi ya kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa barabara hii ili iweze kujengwa kwa kiwango cha lami. Baada ya hatua hiyo kukamilika na gharama za ujenzi kujulikana, Serikali itatafuta fedha za ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Husna Sekiboko.

**MHE. HUSNA J. SEKIBOKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwanza nishukuru kwa majibu ya Mheshimiwa Waziri, lakini nimshukuru sana Waziri Mkuu Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, wakati wa ziara yake katika Jimbo la Mlalo alitoa maelekezo barabara hii kujengwa yote kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ujenzi wa barabara hii upembuzi yakinifu na usanifu wa kina unachukua muda kama ambavyo Mheshimiwa Waziri ameeleza hapo; kwanza, wafanye upembuzi na baadaye itafutwe fedha kwa ajili ya ujenzi.

Sasa wakati hayo maandalizi yote yanafanyika, kwa nini Serikali isi-*release*, isitoe fedha ili kuendelea kutekeleza ule ujenzi wa vipande vipande kama ilivyokuwa awali?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, barabara hii pia ina mzunguko wa kutoka Magamba kwenda Lukozi – Mlalo, lakini mzunguko mwingine ni kutoka Lukozi kupita Manolo kwenda Sunga - Mtae mpaka Lunguza ambapo inakutana na hii *Umba Junction.*

Je, Serikali ina mpango gani wa kuijenga pia barabara hii ya mzunguko wa juu kupitia Mtae kwenda *Umba Junction* kwa kiwango cha lami? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, kwanza, ninashukuru kwa maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Husna Sekiboko, Mbunge wa Viti Maalum, Mkoa wa Tanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninafahamu matamanio ya Mheshimiwa Mbunge ni kuona hatua hizi zote zinakamilika kwa haraka na ujenzi wa kiwango cha lami ambao utawaondolea adha wananchi wa kutoka Lushoto na Mlalo wapate nafuu. Lushoto na Mlalo ambapo Waziri wa TAMISEMI, Mheshimiwa Profesa Riziki Shemdoe na Mbunge wa Mlalo Mheshimiwa Rashid Shangazi wamekuwa wakiipigania sana barabara hii wakati wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka nimhakikishie tu kwamba ameniomba wakati tunaendelea na hatua hizi ule utaratibu wa kutazama walau vipande vidogo vidogo uendelee.

Sasa ninampa *comfort* kwamba nimeelekeza wataalam wangu waniletee nitoe idhini ya kipande cha kilometa 2.4 cha kutoka Nyasa mpaka Majulai katika Jimbo la Mlalo ambalo linawakilishwa na Mheshimiwa Rashid Shangazi, tutahakikisha kwamba tunakwenda kumtafuta mkararasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na kwa kuwa uelekeo wetu mara baada ya bajeti kuu kupita Wakala wetu wa Mfuko wa Barabara Tanzania tunatarajia mambo yatakwenda kuwa mazuri na kwa hiyo, tutafanya kazi ya kutengeneza vipande vile ambavyo vinaonekana ni korofi na sumbufu kwa wananchi ikiwa ni pamoja na Jimbo hili la Mlalo na kule Lushoto kama nilivyotamka mwanzo kutoka Nyasa kwenda Majulai tutawapa kipaumbele kwa mzingatio huu wa Mheshimiwa Husna Sekiboko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile ameniuliza kuhusiana na kipande ambacho hakizungumzwi cha kuelekea Mtae mpaka *Umba Junction* na *Umba Junction* mpaka Mkomazi barabara ambayo inaunganisha na Wilaya ya Same ni barabara muhimu sana. Sasa kwa hiki kipande cha kuelekea Mtae ninatoa maelekezo kwa wataalam wetu wa *TANROADS* hususani wa Mkoa wa Tanga na chenyewe wakianzie kazi maana kile cha

kwenda Magamba kuunganisha na Wilaya ya Mkinga chenyewe tayari kama nilivyojibu katika swali la awali. Kinakwenda vizuri. Sasa tutaelekeza fikra yetu pia upande wa kuelekea Mtae.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimpe uhakika Mheshimiwa Husna Sakiboko na Wanatanga na majirani zao pia vilevile wa upande wa Same - Kilimanjaro kwamba tumelichukuchukua jambo hili na kuitazama barabara ya kuelekea Mtae ili tuweze kuianzia hatua kwa hatua kama ambavyo ile ya kuelekea Magamba tumeipa kipaumbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Adonis Bitegeko.

**MHE. ADONIS A. BITEGEKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa kunipa nafasi kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Wilaya ya Muleba, Jimbo la Muleba Kaskazini kuna barabara za kutoka *Kamachumu Center* kwenda Hospitali ya Ndolage na kutoka Kata ya Nshamba kwenda Kata ya Mushabago katika Kijiji cha Rushwa ambazo tayari zimeshafanyiwa usanifu na *TANROADS* zinasubiri kujengwa kwa kiwango lami. Je, ni lini Serikali itaanza kujenga barabara hizo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nijibu swali hili la wananchi wa Muleba kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimechukua na ninashukuru kwamba hatua ya usanifu imekwisha kupita. Nitoe tu maelekezo kwa Meneja wetu wa *TANROADS* wa Mkoa wa Kagera, *Engineer* Joel aweze kuhakikisha kwamba hatua za awali ikiwa ni pamoja na kuileta sasa upande wa *headquarter* ya *TANROADS* na Wizarani ili tuweze kuitafutia fedha na ili tuweze kuitengeneza barabara hii ya wananchi inayoanzia pale Kamachumu kwa kiwango hiki cha lami pindi upatikanaji wa fedha utakapokuwa mzuri. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Agnesta Lambert.

**MHE. AGNESTA L. KAIZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara kutoka Kifuru kuelekea *Pugu Station* - Mnadani ni barabara ambayo ipo ndani ya Ilani ya Chama Cha Mapinduzi tangu enzi za Hayati Magufuli, na hivi sasa ninavyoongea barabara hii ni mbovu na nimekuwa nikiongea na wewe na umekuwa ukinipa ushirikiano mkubwa sana, ninakushukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa swali langu, ni lini barabara hii mtakwenda kuijenga kwa sababu wananchi wanapata adha kubwa na mifugo inapata adha kubwa kuelekea Pugu Mnadani. Mheshimiwa Waziri, ninaomba tabasamu kwa Wana-Kifuru kuelekea *Pugu Station*. Na nikuombe ukubali kuambatana na mimi baada ya Bunge hili uende kujionea hali halisi jimboni kwangu. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na nashukuru kwa swali la nyongeza la Mheshimiwa Agnesta Lambert, Mbunge wa Jimbo la Segerea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninakubali ombi la kwenda kuambatana naye kuelekea Segerea kwenda kukagua miundombinu ya Jimbo la Segerea. Niko tayari mara baada ya Mkutano huu wa Bajeti kukamilika tutafanya ziara na niwape *comfort* watu wa Segerea, ninafahamu barabara zao nyingi zimepondwapondwa na zimeharibika wakati huu wa mvua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Naibu Waziri wa TAMISEMI na Waziri wa TAMISEMI pia ambapo barabara hizi nyingi zinaangukia upande wa *TARURA*, lakini wamezipangia mpango mzuri. Tuna mradi mkubwa kule wa *DMDP II* ambao Mheshimiwa Agnesta na Wabunge wengine wa Mkoa wa Dar es Salaam

wamekuwa wakiufuatilia kwa karibu sana na kuusisitiza sana. Ninaamini kwa uelekeo huo, Dar es Salaam inakwenda kubadilika kwa kiwango kikubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Agnesta na wana-Dar es Salaam pia msisahau barabara ile ya Mandela kuanzia Ubungo kwenda bandarini tunakwenda kujenga barabara ya kisasa inayounganishwa na mwendokasi, lakini pale *junction* ya Tabata tutajenga *flyover* ili pawe na urahisi na kutoleta msongamano katika eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tukienda Kifuru – Pugu Mnadani, ni kweli kwamba barabara ile ni mbovu na ni barabara muhimu kwa ajili ya watu kwenda kuungana kwenda kupanda treni yetu ya kisasa ya *SGR*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwape *comfort* Wabunge wote, kwenye maeneo ambayo yana vituo vyetu vya *SGR,* mkakati wetu ndani ya Serikali ni kuhakikisha tunafungamanisha. Sisi Wizara ya Ujenzi na Wizara ya Uchukuzi tunazungumza lugha moja ili watu wapate urahisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimefurahi pia asubuhi ya leo nimesikia maswali ya namna hii ikiwa ni pamoja na lile swali la kwetu pale Pwani la kutoka Mlandizi kwenda *Ruvu Station* ambayo tayari mkandarasi tumekwishampata wakati wowote tutamlipa *advance payment*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, kule Tabora kwa Mheshimiwa Bashungwa na Mheshimiwa Luhende wamekuwa wakipigania sana barabara ya kutoka Nzega – Bukene ambayo inakwenda kuwaunganisha na *station* ya *SGR*. Mheshimiwa Bashe amekuwa akihangaika sana na jambo hili muda mrefu na nataka niwape *comfort* ya kwamba tumezungumza na wenzetu wa Wizara ya Uchukuzi tunakwenda kuijenga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale *Pugu Station* ng'ombe wanavunjika miguu kwenye malori kwa sababu ya kipande kile tu. Ni msisitizo wa Rais, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ya kwamba tunajenga barabara hizi na tutazijenga, si tu kwa

sababu ya kujenga kwa sababu ya kupata idadi kubwa ya viwango vya lami, lakini ni kwa kuzingatia tabasamu la utu kwa Watanzania. Tutafanya kazi hiyo kwa weledi mkubwa na uaminifu ili Watanzania waweze kupata huduma iliyo bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakupongeza tena Mheshimiwa Agnesta kwa upambanaji wako wewe na Wabunge wote wa Mkoa wa Dar es Salaam, ni kazi nzuri mnayoifanya, nina hakika tutakwenda kuibadilisha Dar es Salaam na itapendeza sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu hayo ya Waheshimiwa Wabunge kutoka Wizara ya Ujenzi.

Tunaendelea sasa na Wizara ya Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Janeth Elias Mahawanga, Mbunge wa Viti Maalum, aulize swali lake.

Na. 525

**_BRELA_ Kulinda Biashara za Wanawake Wajasiriamali**

**MHE. JANETH E. MAHAWANGA** aliuliza: -

Je, *BRELA* inachukua hatua gani kulinda bidhaa za wanawake dhidi ya wizi wa nembo, chapa au mawazo ya ubunifu?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na Biashara, naomba sasa nijibu swali namba 525 kama lilivyoulizwa na Mheshimiwa Janeth Elias Mahawanga, Mbunge wa Viti Maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia *BRELA* imekuwa ikilinda bidhaa za wafanyabiashara wakiwemo wanawake dhidi ya wizi wa nembo, chapa na mawazo ya ubunifu kupitia usajili wa

alama za biashara na huduma kwa mujibu wa Sheria ya Alama za Biashara na Huduma, Sura Namba 326.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria hii inampa mmiliki haki ya kipekee ya kutumia alama hiyo na kumwezesha kuchukua hatua za kisheria endapo itatumiwa bila idhini yake. Usajili wa alama hizo hufanyika kupitia mfumo wa mtandaoni wa usajili wa *BRELA* ambao unatambulika kama *Online Registration System*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Janeth Mahawanga.

**MHE. JANETH E. MAHAWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali. Pamoja na majibu hayo, nina maswali madogo mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza, kwa kuwa wanawake wengi wanajishughulisha na shughuli za utengenezaji wa bidhaa za chakula, vipodozi na kazi za mikono, je, Serikali imejipangaje kuhakikisha inazilinda bidhaa hizi dhidi ya bidhaa zinazotumia chapa *fake* kwa ajili ya wajasiriamali hawa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, *BRELA* imejipangaje kuhakikisha wanawake wa vijijini wanafikiwa na huduma za chapa na alama za biashara? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza natumia nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Janeth Mahawanga kwa jitihada zake ambazo zimekuwa mkombozi mkubwa kwa wanawake wa Mkoa wa Dar es Salaam na Tanzania kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Viwanda na Biashara kupitia *BRELA* tumekuwa tukitoa elimu kwa wanawake wajasiriamali na kwa mwaka jana pekee tumewafikia wanawake zaidi ya 1,000 katika mikoa 13 ya Tanzania Bara. Mikoa hiyo ni

Shinyanga, Morogoro, Songwe, Ruvuma, Lindi, Mtwara, Pwani, Dodoma, Geita, Simiyu, Manyara na Mara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunawafikiaje wanawake hasa wa vijijini? Shirika la *BRELA* kwa kushirikiana na *SIDO* wamekuwa wakiendesha mafunzo kwa wajasiriamali kwa ajili ya kulinda bunifu, lakini kuwaelezea umuhimu wa usajili wa alama za biashara na mawazo ama bunifu mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, *BRELA* imekuwa ikishiriki matukio mbalimbali kama Sabasaba, Nanenane na maonesho ya taasisi mbalimbali ikielimisha wajasiriamali katika maeneo tofauti ya nchi, lakini pia imekuwa ikitoza usajili wa hapo kwa papo na kazi hii imekuwa ikifanyika katika mikoa mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi la Mheshimiwa Mbunge ni kufika katika Mkoa wa Dar es Salaam na naomba kutumia nafasi hii kumpa faraja Mheshimiwa Mbunge kwamba kuna maelekezo kwa *BRELA* kuanza kutoa elimu hii katika maeneo ya pembezoni mwa Mkoa wa Dar es Salaam na kazi hii imeshaanza na inaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mariam Nyoka.

**MHE. MARIAM M. NYOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru; je, Serikali ina mfumo gani wa kufuatilia na kubaini chapa zinazokiuka hakimiliki za watu wengine kabla ya kusajiliwa? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Sheria ya Alama za Biashara na Huduma, Sura Namba 326 ni kosa kutumia alama za biashara ama miliki bunifu za mtu. Kwa hiyo, elimu ambayo tumekuwa tukiitoa ni kuwaomba wajasiriamali mbalimbali kusajili kwanza miliki bunifu zao, lakini kutupa ushirikiano pale wanapoona

kwamba kuna watu ambao wanaiba ama wanatumia bila idhini ya hawa wamiliki ambao wamesajili bunifu hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale ambapo tunapata taarifa hizo tumekuwa tukishirikiana nao kwa ajili ya kuhakikisha kwamba sheria inachukua mkondo wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Neema Majule.

**MHE. DKT. NEEMA P. MAJULE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naomba kumuuliza Waziri; je, Serikali haioni kwamba ni haja sasa ya kuweka wataalam ili wakawasaidie wanawake kubuni hizo alama, halafu na kupunguza gharama waweze kusajiliwa ili wanawake hao watakapokuwa na alama hizo waweze kuhimili ushindani wa soko la nchi za nje? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyojibu swali la msingi, *SIDO* wamekuwa wakiendesha madarasa haya kwa kufikia makundi mbalimbali hasa wanawake, kwa mfano, madarasa ya *SIDO* yanachukua wanafunzi 40 kwa wiki na *majority* wanakuwa ni wanawake na kwa kuona umuhimu wa kutoa elimu ya kulinda miliki bunifu na alama za biashara, *BRELA* wamekuwa wakishiriki madarasa haya ya *SIDO* na ushirikiano huu umekuwa ukizaa matunda kwa maana wanafikia watu wengi na hasa wa pembezoni. Kazi hii inafanyika kwa umakini na matokeo tunayaona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu hayo ya Waheshimiwa Wabunge kutoka Wizara ya Viwanda na Biashara.

Tunaendelea sasa Wizara ya Fedha, Mheshimiwa Tinnar Andrew Chenge, Mbunge wa Viti Maalum, aulize swali lake.

Na. 526

**Kigezo Kinachotumika Kutoza Kodi ya Majengo**

**MHE. TINNAR A. CHENGE** aliuliza: -

Je, Serikali inatumia kigezo gani katika kutoza Kodi ya Majengo *(Property Tax)* kupitia mfumo wa mita za LUKU nchini?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. LAURENT D. LUSWETULA)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Tinnar Andrew Chenge, Mbunge wa Viti Maalum.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa Serikali inatumia viwango mfuto katika kutoza kodi za majengo kupitia mita za umeme za LUKU. Vigezo vinavyotumika kutoza kodi za majengo kupitia LUKU ni kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja; nyumba ya kawaida ambayo inatozwa shilingi 18,000 kwa mwaka au shilingi 1,500 kwa mwezi; na nyumba ya ghorofa ambayo inatozwa shilingi 90,000 kwa kila sakafu kwa mwaka au shilingi 7,500 kwa kila sakafu kwa mwezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nyumba za nyasi, udongo, huduma za jamii, kuabudia na anayoishi wazee kuanzia miaka 60 hazitozwi kodi ya majengo isipokuwa endapo majengo hayo ni ya kibiashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Tinnar Chenge.

**MHE. TINNAR A. CHENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na nashukuru majibu mazuri ya Serikali, lakini nina maswali madogo mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza, kwa kuwa kodi hii ya *property tax* inapaswa kulipwa na mmiliki wa jengo na kwa kuwa kuna wajasiriamali ambao wamepanga kwenye *frame* za maduka zinazomilikiwa na wafanyabiashara na kwenye *frame* hizi zimefungwa LUKU. Je, ni kwa nini Serikali inawakata *property tax* wajasiriamali hawa kwenye mita hizi za LUKU? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; je, Serikali haioni haja kwamba kuna umuhimu sasa wa kuipitia sera hii ili mmiliki wa jengo huyu alipe kodi hii kupitia kwenye mita yake ya LUKU badala ya kumbebesha mzigo mjasiriamali huyu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. LAURENT D. LUSWETULA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza namshukuru sana Mheshimiwa Tinnar Andrew Chenge na kuendelea kuwapongeza sana wanawake wa Mkoa wa Simiyu kwa kutuletea mtu huyu makini na bora ambaye anajenga hoja za kujenga hapa Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikija kwenye maswali ya nyongeza, yako mawili lakini yenye namna moja ni kama yanashabihiana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kwanza kama Serikali naweze kukiri kabisa, kwa sasa hivi utaratibu unaotumika ndiyo huu ambao Mheshimiwa Tinnar ameuzungumza kwamba inalipwa kupitia LUKU ambapo watumiaji sasa wa LUKU ndiyo wanaolipa. Watumiaji wa LUKU hawa ndiyo wanaweza wakawa ni wamiliki au wanaweza wakawa wapangaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa wapangaji, ndiyo maana tumeliona hili kama Serikali na sisi kwa kushirikiana na

wenzetu Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI ambapo sasa kwamba hizi halmashauri ziko chini yao, tumekaa na tumechakata na tunaendelea kuchakata kuona namna bora zaidi ambayo sasa tutakusanya kodi hii ya majengo kwa wamiliki na siyo wale wapangaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zacharia Paulo.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, bado kuna haja ya kufanya zoezi hili kwa marejeo katika kipindi fulani fulani kwa ajili ya majengo na matumizi kubadilika mara kwa mara.

Je, Serikali haioni kuwa kuna haja sasa ya kufanya marejeo ya uhakiki wa majengo hayo hasa yale ya wananchi wa makundi ya chini ambayo taratibu zinawataja wasitozwe?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. LAURENT D. LUSWETULA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na ninampongeza sana Mheshimiwa Mbunge kwa swali lake la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza na mimi nakiri kabisa na nasema ya kwamba kodi hizi za majengo kwa maana ya *property tax* zinakusanywa na halmashauri kupitia shirika letu la umeme *TANESCO* ambazo maana yake hizi ni nyumba ambazo zimeunganishwa na umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nyumba ambazo pia hazijaunganishwa na umeme, bado halmashauri zetu zimeendelea kukusanya kwa *rate* ile ile kulingana na mwongozo unavyotuongoza. Kwa namna hiyo, sisi kama Serikali tumejipanga kabisa na ukiangalia namna mfumo ulivyo, tumejipanga kuhakikisha kwamba halmashauri zetu kwanza zinakusanya kodi hii bila upendeleo, kumpendelea mtu yeyote au nyumba yoyote na ndiyo maana kama mpango wa Serikali kupitia kwa

kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, mpaka sasa hivi wale watendaji wetu wa vijiji tumeweza kuwawezesha vishkwambi kwa ajili ya kusajili nyumba ambazo hazijasajiliwa mpaka sasa hivi na hazilipi kodi ya majengo. Tumewawezesha na zoezi hilo linaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hilo, tumewawezesha pia mfumo ambao watakuwa na uwezo wa kutoa *control number* kupitia vile vishkwambi. Kwa namna hiyo, na mimi natumia fursa hii hii kuwaasa wananchi wote ambao tayari wameshapewa zile *control number* kuweza kuzilipia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Simon Lusengekile.

**MHE. SIMON S. LUSENGEKILE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi niulize swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wamekuwa wakimaliza ujenzi wa nyumba zao baada ya mwaka wa fedha kuwa umeanza, kwa mfano, mwananchi anamaliza kujenga nyumba yake mwezi huu Juni na kuingiza umeme kwa mara ya kwanza lakini amekuwa akikatwa kuanzia mwezi Julai mwaka jana mwaka wa fedha ulivyoanza na kumsababishia madeni ambayo siyo ya msingi kwake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Serikali ina hatua gani kuhakikisha kwamba sasa wananchi wanakatwa kulingana na muda ambao amemaliza ujenzi na kuweka LUKU yake kwenye nyumba yake? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. LAURENT D. LUSWETULA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, kwanza nampongeza sana kaka yangu na Mheshimiwa kwa swali lingine zuri kabisa la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nasema tu natumia nafasi hii kusema kwamba mapendekezo yake tumeyapokea kama Serikali. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa *Engineer* Fadhili.

**MHE. ENG. FADHILI S. CHILOMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upo mkanganyiko umekuwa ukijitokeza kwenye majengo mengi na hasa kupitia hii kodi. Unakuta jengo moja labda la ghorofa lina mita zaidi ya tano au 10 au 20 kutegemea na ukubwa wa jengo lenyewe. Mtazamo unaoonekana ni kwamba kila kwenye mita pana nyumba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili limeleta kero kubwa sana kwa wananchi; je, Serikali haioni haja sasa ya kufanya upembuzi yakinifu kuona kwamba ni wapi kuna nyumba, ni wapi hakuna nyumba na nyumba ziko ngapi ili kuondoa kero hiyo kwa wananchi? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. LAURENT D. LUSWETULA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa nafasi hii na kwanza, nampongeza sana Mheshimiwa Mbunge na kwa namna alivyotoa hoja yake ni kama anatoa maoni kwa Serikali. Nasema kwamba maoni yake tumeyapokea na tutayafanyia kazi. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu hayo ya Waheshimiwa Wabunge kutoka Wizara ya Fedha.

Tunaendelea sasa Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mheshimiwa Masache Njelu Kasaka, Mbunge wa Lupa, aulize swali lake.

Na. 527

**Ujenzi wa Mnara wa Simu Kijiji cha Shoga**

**MHE. MASACHE N. KASAKA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itajenga mnara katika Kijiji cha Shoga ili kutatua changamoto ya mawasiliano ya simu?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Masache Njelu Kasaka, Mbunge wa Jimbo la Lupa, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Wizara Mawasiliano na Teknolojia ya Habari inaendelea kuboresha huduma za mawasiliano nchini kwa kutatua changamoto za huduma ya mawasiliano katika maeneo mbalimbali katika Kijiji cha Shoga. Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kupitia Shirika la Mawasiliano Tanzania kupitia Awamu ya Tisa Mradi wa Mawasiliano Vijijini inaendelea kutekeleza ujenzi wa mnara wa mawasiliano katika eneo la *Shoga Pitch* ambapo utekelezaji wake unatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwezi Juni, 2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 13 Mei, 2026 Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote kwa kushirikiana Ofisi ya Mbunge wa Jimbo la Lupa pamoja na viongozi wa Kijiji cha Shoga ilifanya ziara na kujionea maendeleo ya ujenzi wa mnara huo ambapo mkandarasi, Kampuni ya Huawei Tanzania ameahidi kukamilisha ujenzi ifikapo mwishoni mwa mwezi Juni, 2026 ili kutatua changamoto ya mawasiliano yaliyopo katika kijiji hicho cha Shoga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Masache Kasaka.

Zima *microphone* na washa tena au wengine wapunguze *microphones* zimewaka nyingi sana. Jaribu kuwasha tena.

Jaribu kuwasha tena, ulizia hapo nyuma, ulizia kwa Mheshimiwa jirani yako hapo. Tayari?

**MHE. MASACHE N. KASAKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi, lakini pia ninashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kuweza kuipongeza Serikali Kijiji hiki cha Shoga tayari mnara huu wa mawasiliano umeshawaka, na pamoja na mnara huu, na vijiji vingine Kijiji cha Mlemanjiwa, Kijiji cha Igundu, Kijiji cha Mkora, Upendo na Sipa mwezi uliopita wa tano na kwenyewe minara hii ya mawasiliano imewaka. kwa hiyo tunaishukuru sana Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, nina maswali madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo mengi ya Wilaya ya Chunya ambako ni maeneo ya wachimbaji wadogo yana changamoto kubwa sana ya mawasiliano kiasi kwamba wachimbaji wetu wanapata shida kubwa wanapokuwa maeneo yao ya kazi.

Je, ni upi sasa mpango wa Serikali kuhakikisha kwamba maeneo haya ya wachimbaji wadogo yanaweza kupata mawasiliano ya uhakika ili na wao watumie fursa hii kujitafutia kipato chao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, pale Chunya Mjini tuna changamoto kubwa sana ya mawasiliano hasa mnara wa Vodacom kiasi kwamba mawasiliano yamekuwa ni magumu na mtandao wa *internet* umekuwa ni changamoto kubwa sana.

Je, ni upi mpango wa Serikali sasa kushirikiana na kampuni ya Vodacom kuhakikisha kwamba unaongeza mnara wa mawasiliano pale Chunya Mjini ili mawasiliano yawe ya uhakika?

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Kasaka kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninaanza kumpongeza kwa kuwa mfuatiliaji mzuri wa sekta hii ya mawasiliano. amekuwa akitufuatilia kwa karibu sana, Mheshimiwa Waziri na mimi, amekuwa akija Wizarani kufuatilia, kwa kweli anawapigania sana wananchi wa jimbo lake, hongera sana Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali la kwanza la maeneo mengi kukosa mtandao hususan katika maeneo ya wachimbaji wadogo, ninapenda kumjulisha Mheshimiwa Mbunge kwamba kuna mradi tunaoutekeleza sasa hivi awamu ya 10 ambao tulisaini mkataba mwezi Disemba, 2025 na unategemea kukamilika mwezi Machi, 2027. Katika jimbo lake tutajenga minara minne kwenye Kata za Bwawani ambapo mtoa huduma Vodacom watajenga, Kata ya Lupa itajengwa na mto huduma Airtel, Kata ya Mamba Vodacom na Kata ya Mtanila atajenga Airtel.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya umuhimu wa sekta hii ya uchimbaji mdogo mdogo, ninamwelekeza Mkurugenzi Mkuu wa *UCSAF* kupitia katika maeneo yote ambayo kuna wachimbaji wadogo wadogo kufanya tathmini, tuangalie tunaweza kufanya nini kama hatua ya dharura kuhakikisha kwamba katika maeneo haya ya wachimbaji wadogo wadogo ambayo ni muhimu katika uchumi wa nchi yetu, wanapata mawasiliano ya uhakika ili waweze kufanya kazi yao kwa uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali lake la pili la changamoto ya mawasiliano katika Mji wa Chunya Mjini, ninamwelekeza Mkurugenzi Mkuu wa *TCRA* kufanya tathmini katika Mji huo wa Chunya kuona kwamba huo mnara uliopo wa Vodacom una tatizo gani. Kama umeelemewa, basi waangalie

uwezekano wa kuongezea nguvu ili mawasiliano yapatikane ya uhakika na kama kunahitajika kujenga mnara mwingine, basi taarifa hiyo iletwe Wizarani ili tuwaelekeze *UCSAF* kuanza mchakato wa kuangalia namna wanavyotatua tatizo hilo kwa kujenga mnara mwingine. Ninakushukuru.

**MWENYEKITI:** Ninaona *microphones* zina tatizo kidogo. Ninamwona Mheshimiwa Mecktridis Mdaku, Mheshimiwa Joseph Kamonga.

**MHE. MECKTRIDIS F. MDAKU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na changamoto kubwa sana ya mawasiliano katika maeneo ya Jimbo la Malinyi hususan katika Kata za Usangule, Mtimbira, Biro pamoja na Ngoeranga.

Je, ni lini Serikali itakwenda kujenga minara katika maeneo yao hayo ili wananchi waweze kupata huduma ya mawasiliano?

**MWENYEKITI:** Majibu kwa ufupi, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara inatekeleza mpango wa miaka mitano wa ujenzi wa minara katika maeneo yote yenye changamoto ya minara hapa nchini. Kwa hiyo, ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba katika mpango wetu huu, tutayafikia maeneo yote yenye changamoto ya umeme yakiwemo maeneo aliyoyataja hayo. Kwa hiyo, mpango wetu huu wa miaka mitano unakusudia kutatua kwa kiasi kikubwa changamoto ya mawasiliano nchini kama sio kuyamaliza kabisa. Nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Joseph Kamoga, nimemuona pia Mheshimiwa Yannick Ndoinyo. Aanze kuuliza Mheshimiwa Yannick Ndoinyo wakati wewe unajiandaa.

**MHE. YANNICK I. NDOINYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni nini mpango wa Serikali wa kusambaza minara ya mawasiliano katika Kata za Wilaya ya Ngorongoro hasa zile ambazo ziko pembezoni mwa njia kuu? Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge wa Ngorongoro, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango wa Serikali kusambaza minara nimewaeleza kwamba uko katika mpango wetu wa miaka mitano wa kuhakikisha kwamba tunatatua changamoto ya mawasiliano katika nchi hii, tunaitatua au tunaimaliza kabisa, na katika maeneo ya mpakani, tuna mradi wa awamu ya 11 ambao utajikita katika ujenzi wa minara katika maeneo ya mpakani, maeneo ya reli, maeneo ya *SGR*, *MGR*, *TAZARA* na maeneo maeneo yote ya kimkakati ya mpakani ambayo yote tutayajenga katika awamu ijao ya awamu ya 11 ambayo iko katika hatua ya manunuzi hivi sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwenye maeneo yote yenye changamoto, tutayashughulikia awamu ya 11 ambayo iko kwenye awamu ya ya manunuzi. Hatua ya manunuzi na mengine yatakayobaki tutayatekeleza katika mpango wetu wa miaka mitano wa ujenzi wa minara nchi nzima. Ninakushukuru.

**MWENYEKITI:** Ninaona hapa Mheshimiwa Florent Kyombo na Mheshimiwa Ritta Kabati, Mheshimiwa Liwaka jaribu kutafuta *microphpone* sehemu nyingine.

**MHE. FLORENT L. KYOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninaipongeza Serikali imejenga minara kama mitano ndani ya Jimbo la Misenyi, lakini

bado vijiji mbalimbali ndani ya Kata za Bugandika, Kitobo, Minziro na maeneo mengine bado tuna shida ya mtandao.

Je, ni lini sasa tutakamilisha ujenzi wa minara hiyo ili wananchi wote waweze kupata mawasiliano kwa sababu ya shughuli za kiuchumi?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu swali la Mbunge wa Misenyi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba changamoto ya mawasiliano katika jimbo lako tunaitambua na jimbo lako pia liko katika mpango wetu wa mkakati wa miaka mitano ya ujenzi wa minara. Kwa hiyo ninaomba tu tuendelee kuwa na subira, tutakuwa tunaijenga hii minara kwa awamu katika miaka hii mitano. Ifikapo mwaka 2030 tunaamini kwamba changamoto ya mawasiliano nchi nzima tutakuwa tumeitatua.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Ritta Kabati.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa katika Jimbo la Kilolo kuna baadhi ya vijiji vya Kata ya Kimala, Masisiwe, Ibumu, Mlafu, Udekwa, Ruaha Mbuyuni, Nyanzwa, Mahenge, Ihimbo na Kijiji cha Kiwili, haya maeneo, vijiji hivi havina mawasiliano kabisa na bahati mbaya sana hata miundombinu ya barabara siyo mizuri. Je, Mheshimiwa Waziri upo tayari sasa kuja katika Jimbo la Kilolo ili uje uone wananchi wa vijiji hivi wanavyopata shida?

**MWENYEKITI:** Majibu kwa ufupi, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nijibu swali la Mheshimiwa Ritta Kabati, Mbunge Kilolo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimhakikishie Mheshimiwa Ritta kwamba niko tayari kuandamana naye kwenda katika jimbo lake kufanya tathmini na kujionea changamoto ya mawasiliano katika jimbo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kata alizozitaja, nimhakikishie kwamba tunalipa umuhimu mkubwa suala la mawasiliano nchini na ninapenda kumwelekeza kupitia Bunge lako Tukufu, Mkurugenzi Mkuu wa *UCSAF* kwenda katika Jimbo la Kilolo kufanya tathmini ya changamoto, amesema hakuna mawasiliano kabisa. Kwa hiyo, twende tufanye tathmini, tuone ni hatua gani za dharura tunaweza kufanya, lakini katika awamu ya 10, kuna mnara utajengwa katika Kata moja ya Mlafu na mnara mwingine utajengwa katika Kata ya Ukwega katika jimbo lake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo kata nyingine zilizobaki ambazo amezitaja kata nane zilizobaki, ninamwelekeza Mkurugenzi Mkuu wa *UCSAF* aende kulifanyia kazi suala hili mapema iwezekanavyo. Ninakushukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Fadhili Ngajilo, Mheshimiwa Asia Halamga, maswali mafupi ya nyongeza.

**MHE. FADHILI F. NGAJILO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru pia kwa kupewa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, ninaomba tusikilizane, sauti zinazidi.

**MHE. FADHILI F. NGALIJO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuchukua nafasi hii kukushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi kwangu Jimbo la Iringa Mjini siyo kwamba tuna tatizo la minara, minara ipo, lakini haina nguvu. Kwa hiyo, ninaomba uangalie namna ya kufika kwenye maeneo ya ya Ugele, Msisina, Mtaragala, Kigonzile, Mkoga, Kitasengwa pamoja na eneo ambalo linaitwa Mosi, Mtaa wa Mosi liliopo Kata ya Kitwiru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa swali, je, Mheshimiwa Waziri unaweza sasa ukatuma wataalam wako wakaenda kufanya tathmini na kuhakikisha kwamba mawasiliano yanapatikana hasa eneo lile linalozunguka Uwanja wa Ndege wa Nduli ambao Mheshimiwa Dkt. Samia ameweka pale zaidi ya shilingi bilioni 63?

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge wa Iringa Mjini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawaelekeza na ninamwelekeza Mkurugenzi Mkuu wa *TCRA* apeleke wataalam wake kufanya tathmini katika eneo hili la Iringa Mjini ili kujua chanzo cha tatizo hilo ni nini na kama ni kuongezea nguvu minara iliyopo ambayo amesema ipo, basi awasiliane na watoa huduma ili wakamilishe hiyo kazi. Nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Asia Halamga.

**MHE. ASIA A. HALAMGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaishukuru sana Serikali kwa kunipa minara nane ya mawasiliano, lakini bado nina changamoto kwa kata ya Sirop pamoja na Kata ya Dawar hakuna kabisa minara ya mawasiliano. *(Makofi)*

Je, ni lini Serikali sasa itanipa katika kata hizi mbili minara ya mawasiliano kwa sababu hakuna mnara wowote pamoja na maeneo mengine ya Jimbo la Hanang yenye changamoto?

**MWENYEKITI:** Majibu Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Asia, Mbunge wa Hanang, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli katika awamu ya 10 hii tunajenga minara minane katika jimbo lake katika kata nane na bado kuna kata zina changamoto. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba katika mpango wetu wa miaka mitano wa ujenzi wa minara na hizo kata tutazifikia.

Kwa hiyo, ninaomba aendelee kuvuta subira tukamilishe kwanza hii minara minane tunayoijenga halafu tuendelee kushughulikia na hizo kata zingine ambazo zina changamoto. Ninakushukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Joseph Kamonga, swali fupi la nyongeza. Ninaomba maswali yawe mafupi ili mpate wengi.

**MHE. JOSEPH Z. KAMONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule Ludewa Tarafa ya Mwambao ambayo ina kata zaidi ya tano kuna changamoto kubwa sana ya mawasiliano. Ninashukuru Serikali ilishaenda Makonde na Nsisi, hadi wananchi wameshatoa maeneo, lakini minara haijaanza kujengwa. Ni lini sasa wataalam watakwenda kwa ajili ya ujenzi wa minara hiyo? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Kamonga, Mbunge wa Ludewa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamwelekeze tu Mkurugenzi Mkuu wa *UCSAF* aende kule Ludewa kufanya tathmini ya changamoto ya mawasiliano iliyopo na kuchukua hatua zinazostahili. Ninakushukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Christina Mndeme, Mheshimiwa Esther Midimu na Mheshimiwa Festo Sanga, maswali mafupi ya nyongeza.

**MHE. CHRISTINA S. MNDEME:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, kwa kuwa Serikali imekuwa ikiendelea kuwafikishia wananchi mawasiliano ya simu ikiwemo kuwajengea minara, tunaipongeza sana Serikali; na kwa kuwa pamoja na juhudi nzuri za Serikali, lakini bado maeneo mengine ndani ya Mkoa wa Tabora hayana mawasiliano ya simu.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwapelekea mawasiliano wananchi wa Kata za Igulungu, Makazi, Kijiji cha Katunda, Kata ya Mabama, Kata ya Ibili, Wilaya ya Uyui, Kata za Nhwande, Kata ya Igwisi, Kata ya Ukumbi Siganga, Kata ya Ugunga, Wilaya ya Kaliua na Kata za kabila, Ikomwa, Kakola, Mtalikwa na Ndevelwa Kijiji cha Ng'ombe zilizopo Manispaa ya Tabora? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu swali Mheshimiwa Mndeme, Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Tabora kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizo kata zote alizozitaja tumeziingiza katika mpango wetu wa miaka mitano wa ujenzi wa minara nchi nzima. Kwa hiyo, katika kipindi hiki cha miaka hii mitano, kata zote hizo tutazifikia pamoja na kata zote za Waheshimiwa Wabunge waliomo katika Bunge lako Tukufu kote nchini. Ninakushukuru.

**MWENYEKITI:** Nilimtaja Mheshimiwa Esther Midimu na Mheshimiwa Festo Sanga.

**MHE. ESTHER L. MIDIMU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kijiji cha Kijirishi, Kata ya Mkula Wilaya ya Busega hakina mawasiliano kabisa. Ni lini Serikali itajenga mnara wa mawasiliano katika kijiji hicho?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hivyo kijiji alichokitaja na chenyewe tumekihusisha katika mpango wetu wa miaka mitano wa ujenzi wa minara nchi hii. Kwa hiyo, katika kipindi hiki cha miaka hii mitano tutavifikia vijiji vyote awamu kwa awamu, hatua kwa hatua na kuhakikisha kwamba tutakapofika mwaka 2030 kila eneo lenye changamoto ya mawasiliano nchini tutakuwa tumelifikia. Nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Festo Sanga.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, unaweza ukaona kwamba idadi ya Wabunge wanaoomba minara ni wengi na Serikali kwa nyakati tofauti mmekuwa mkionyeshwa kwamba mna *interest* ya kufunga *satellite* ili tuachane na biashara ya minara. Upi mkakato wa Serikali na umefikia hatua ipi kwenye ujenzi wa kupatikana kwa *satellite* nchini ili mawasiliano yapatikane nchi nzima?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, swali la ujumla hilo. Sasa utatusaidia.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Sanga kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mpango wa Serikali kupata *satellite*, mpango huu tunaendelea nao na katika mwaka ujao wa fedha katika hii bajeti mliyotupitishia mpango huu tutautekeleza. Ninakushukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Fadhili Liwaka nilikutaja.

**MHE. FADHILI A. LIWAKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru, wananchi wa Kilimarondo na Kiegei wanatembea umbali wa kilometa 126 kufuata huduma ya kifedha inayotokana

na mitandao ya simu. Je, Serikali ina mkakati gani kuwajengea minara ya uhakika ili kupata huduma hiyo?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nijibu swali la Mheshimiwa Fadhili Liwaka kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo hayo aliyoyataja kama nilivyoeleza awali yote yako katika mpango mkakati wa Serikali wa Miaka Mitano wa Ujenzi wa Minara katika maeneo yote yenye changamoto hapa nchini.

Kwa hiyo, ninamhakikishia Mheshimiwa Fadhili kwamba maeneo yote aliyoyataja hayo tutayafikia katika kipindi hiki cha mkakati huu kwa sababu tunakwenda hatua kwa hatua kulingana na upatikanaji wa fedha. Kwa hiyo, kadri fedha inavyopatikana, tutakuwa tunatekeleza mkakati wetu na tunategemea kwamba ifikapo mwaka 2030 changamoto ya mawasiliano nchini itakuwa tumeitatua au tumeimaliza kabisa.

**MWENYEKITI:** Ninakushukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu hayo ya Waheshimiwa Wabunge, kwa kweli umejibu maswali mengi na naamini kabisa kwamba dhamira ya Serikali ni kusambaza mawasiliano, minara ya mawasiliano nchi nzima kama jibu lako la mwisho ulivyojibu. Ninaamini Waheshimiwa Wabunge wameridhika, maswali yote yamejibiwa na Mheshimiwa Waziri kuhusu minara.

Tunamalizia sasa na Wizara ya Uchukuzi, Mheshimiwa Grace Elias Nkoma, Mbunge wa Viti Maalum, aulize swali lake.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Grace Elias Mkoma. *(Makofi)*

Na. 528

**Ujenzi wa Uwanja Mkubwa wa Ndege Singida**

**MHE. GRACE E. MKOMA** aliuliza:-

Je, lini Serikali itajenga uwanja mkubwa wa ndege Singida?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Uchukuzi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Grace Elias Mkoma, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeanza utekelezaji wa hatua za awali za uthamini wa mali za wananchi wanaozunguka eneo la Kiwanja cha Ndege cha Singida, kwa lengo la kuwezesha upatikanaji wa eneo stahiki kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo. Zoezi hili linafanyika kwa kuzingatia kikamilifu matakwa ya sheria, kanuni na taratibu za nchi, ili kulinda haki na stahiki za wananchi husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mara baada ya kukamilika kwa taratibu za utwaaji wa eneo hilo, Serikali itaanza hatua zinazofuata za maandalizi ya utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa kiwanja hicho, ikiwemo upatikanaji wa rasilimali fedha kwa lengo la kuboresha huduma za usafiri wa anga, kuongeza fursa za kiuchumi na kuimarisha maendeleo ya Mkoa wa Singida na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Grace Elias Mkoma.

**MHE. GRACE E. MKOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Je, ni lini mchakato rasmi utakamilika ili uwanja wa ndege wa Mkoa wa Singida uweze kujengwa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili, nini mkakati wa Serikali kufungua anga ili sasa ndege yetu ya *Air Tanzania* ili iweze

kusafiri mfano katika nchi za Morocco, Uturuki na Vietnam kwa sababu nchi hizo zina fursa za kiuchumi? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Uchuzi napenda kujibu maswali ya nyongeza mawili ya Mheshimiwa Grace Elias Mkoma, Mbunge wa Viti Maalum kama ambavyo ameulizia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza nampongeza Mheshimiwa Grace Mkoma kwa kutambua umuhimu wa Uwanja wa Ndege wa Mkoa wa Singida na kuendelea kuwa sauti makini ya wanawake na viongozi na wananchi na hii ni kutokana na ukweli kwamba Mheshimiwa Grace anatambua kwamba Mkoa wa Singida kwanza uwanja wake ni mbadala na ni sehemu ya jirani kutoka Dar es Salaam, lakini pia kuna fursa za madini, kilimo, ufungaji pamoja na mambo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Grace Mkoma na wananchi wote wa Mkoa wa Singida kwamba Serikali kwa kutambua umuhimu wa uwanja huu wa Singida imekwishaanza kwanza kwa kutambua eneo kama nilivyosema na hatua inayofuatia sasa ni kukamilisha taratibu za utwaaji wa ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na hivi navyozungumza katika bajeti iliyosomwa hapa Bungeni mwezi huu wa tano na Waziri wa Uchukuzi, Mheshimiwa Mbarawa Makame Mnyaa amewahakikishia Wana-Singida katika mwaka wa fedha 2026/2027 tunakwenda kuanza taratibu mbalimbali kwa ajili ya kuanza utekelezaji wa mradi huo. Nimuombe Mheshimiwa Grace awe na uvumilivu wakati Serikali inafanyia kazi jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; pia nampongeza kwa kuendelea kupigania ndege yetu Shirika letu la *Air Tanzania* ambalo ndiyo shirika kubwa kwa nchi yetu na la Serikali ameuliza ni mkakati gani uliowekwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza kabisa mkakati wa kwanza ni kuingiza kwenye Ilani ya CCM, Serikali ya CCM kupitia aliyekuwa mgombea ambaye ndiye Rais wa nchi, aliwaambia Watanzania anakwenda kuongeza ndege zilizokuwepo na zitakazokuwepo ili ziweze kuwa nyingi zaidi; zaidi ya ndege nane katika kipindi cha miaka mitano hii ijayo hii ni kuongeza uwezo wetu wa kutoa huduma, lakini pia ili kuhakikisha kwamba jambo hili linakwenda kutekelezeka mwaka wa fedha wa 2026/2027 Serikali imejipangia kwenda kuongeza mtandao huo kutoka safari za ndani na nje na za kimataifa 33 zilizopo mpaka kufika 47.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ambapo ukiangalia hadhi iliyokuwepo miaka kumi iliyopita na sasa unaona kabisa vituo vingi vinaongezeka na hapa Bungeni mmesikia matamko ya Wizara jinsi ambavyo tunaongeza ndani ya nchi, tunakwenda Geita tunaunganisha Mwanza na Dodoma na maeneo mengine, pamoja na maeneo mengine ya nje ya nchi ikiwemo visiwa Sychelles na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali inayo mpango wa kwenda mahali pengi zaidi ili kuhakikisha kwamba tunanufaika na fursa ambazo ziko kwenye nchi yetu, lakini mwisho tutaendelea kushirikiana na sekta binafsi kuhakikisha kwamba shirika letu linakwenda kuongeza mtandao zaidi ndani na nje ya nchi yetu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Esther Matiko.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, ukizingatia Wilaya ya Tarime ina nafasi kubwa kama lango muhimu la shughuli za madini, biashara za mpakani lakini zaidi za utalii wa kaskazini mwa Tanzania.

Je, Serikali haioni umuhimu wa kuendeleza *airstrips* ya Magena kuwa kituo cha kisasa cha usafiri wa anga kwa kuweza kuboresha njia ya kurukia ndege, kujenga jengo la abiria na huduma nyingine muhimu ili kuongeza ushindani wa kiuchumi na kuvutia wawekezaji wengi katika eneo hili ambapo wataongeza mapato na kuongeza ajira katika Mji wa Tarime na Tanzania kwa ujumla?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi nipende kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Esther Matiko ambaye ametaka kufahamu *airstrips* ya Magena.

Kwanza ni mpango wa Serikali kuhakikisha kwamba inaboresha viwanja vya ndege mbalimbali takribani 235 vinavyomilikiwa na taasisi za umma sambamba na kuhamasisha ambavyo vinamilikiwa na taasisi binafsi na katika hivyo vikiwemo 61 vinavyomilikiwa na *TAA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimuombe Mheshimiwa Mbunge tupokee ushauri wa *airstrips* aliyoisema kwa sababu katika mkoa wake pale Serikali inakwenda kujenga uwanja wa ndege mkubwa wa Serengeti katika mkoa huo huo, Musoma Mjini tunajenga uwanja wa ndege wa Musoma. Kwa hiyo, inawezekana tusifike haraka kwenye hiyo *airstrip* aliyoisema, lakini awe na subira tutaipokea na kulichakata na kulingana na upatikanaji wa fedha na taratibu Serikalini tutakwenda kufanyia kazi katika muda mwafaka.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Rashid Mtima, ajiandae Mheshimiwa Neema Mgaya.

**MHE. RASHID M. MTIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi kuuliza swali la nyongeza.

Ni lini Serikali itatimiza ahadi yake ya kujenga uwanja wa ndege eneo la Luchingu, Newala Mjini baada ya kuruhusu kiwanja cha zamani pale Nangwala kupima viwanja? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali inayo dhamira ya kuujenga uwanja husika mara tutakapokamilisha taratibu za utwaaji wa ardhi kwa maana ya vifaa vya fidia basi tutakwenda kuanza mchakato huo wa ujenzi

wa uwanja ili wananchi waweze kunufaika na fursa zilizopo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Neema Mgaya, Mheshimiwa Josephine Kapoma ajiandae.

**MHE. NEEMA W. MGAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, takribani miaka kumi na tano sasa ndani ya Bunge hili nimekuwa nikiuliza lini Serikali itajenga Uwanja wa Ndege wa Njombe?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini? Kwanza Mkoa wa Njombe ndiyo mkoa ambao unalima parachichi kwa wingi na kila siku tunasisitiza, tuna hamasisha wawekezaji waje kuwekeza ndani ya mkoa wetu. Je, tunawezaje tukahamasisha wawekezaji waje kuwekeza ndani ya mkoa wetu ili hali hatuna uwanja wa ndege wa Njombe je, Serikali lini mtajenga uwanja huu wa Njombe? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Neema Mgaya kuhusiana na Uwanja wa Ndege wa Njombe, nimhakikishie Waziri wa Uchukuzi, Mheshimiwa Mbarawa amenituma niwaambie Waheshimiwa Wabunge kwamba uwanja wa ndege ni uwanja muhimu na mara kadhaa hapa Bungeni limekuwa likiulizwa swali hilo sambamba na Uwanja wa Ndege wa Tiabajwa, Serengeti na wa Mwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2026/2027 zimetengwa fedha kwa ajili maendelezo mbalimbali. Kwa sasa tupo kwenye hatua ya kutwaa ardhi tutakapokamilisha tutakwenda kwenye hatua ya pili kwa ajili ya kuanza kuujenga uwanja huo ambao ni muhimu siyo tu kwa ajili ya kilimo cha parachichi na kusafirisha mazao ya mboga mboga, lakini ninyi mnafahamu Njombe ni *center,* Njombe tuna mradi mkubwa sana wa Liganga na Mchuchuma ambao tunategemea kwamba wananchi pamoja na wawekezaji mbalimbali wanahitaji kuutumia.

**MWENYEKITI:** Nilimtaja Mheshimiwa Josephine Kapoma.

**MHE. JOSEPHINE J. KAPOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kati ya vipaumbele vikubwa vya kuongeza uchumi Mkoa wa Morogoro ikiwa kimoja wapo ni kuongeza idadi ya watalii wa ndani kutoka watalii 60,000 mpaka 300,000 na wa nje kutoka 400,000 mpaka 750,000 na Serikali ilishatuahidi kutujengea kiwanja cha ndege kwenye Hifadhi ya Mbuga ya Mikumi; je, ni lini Serikali itaanza kutekeleza suala hili? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Josephine kwa swali lake ambalo kimsingi ameliuliza. Ni kweli Serikali inayo dhamira ya dhati ya kuendeleza sekta ya utalii na uwanja wa ndege pale Mikumi ni moja ya vipaumbele vyetu kwenye ilani yetu. Nimhakikishie kwa kuwa ndiyo tunaanza utekelezaji wa ilani hiyo, aipe muda Serikali iendelee na mchakato wa ndani, tutakapokuwa tayari basi tutakwenda kuanza taratibu za kuujenga uwanja huo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zainab Kawawa, ajiandae Mheshimiwa Kawamba Mustapha.

**MHE. ZAINAB R. KAWAWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kuniona. Ukisoma ile *investment guide* inaonesha namna gani Mkoa wetu wa Lindi ni mkoa wa kimkakati hasa kiuchumi, lakini pia una historia nzuri ya kutafuta kupambania uhuru wa nchi mbalimbali za Kiafrika, ina vivutio vya bahari, ina ardhi nzuri ya uwekezaji, inavutia kwenye kilimo pamoja na vivutio vya utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninafahamu kwamba Sera ya Serikali ya CCM inayoongozwa na Rais Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ni kujenga viwanja vikubwa katika kila mkoa wa nchi yetu ya Tanzania.

Sasa je, kwa vivutio hivi ambavyo vipo katika mkoa wetu wa Lindi; ni lini Serikali itajenga kiwanja kikubwa cha ndege katika Mkoa wa Lindi? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Uchukuzi napenda kumjibu Mheshimiwa Zainab Kawawa ambaye anataka kufahamu ni lini Uwanja wa Ndege wa Lindi utajengwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nakubaliana naye na kumpongeza Uwanja wa Ndege wa Lindi ni uwanja umuhimu kiuchumi kama alivyosema kutokana na uzalishaji wa mazao ya kibiashara kama vile korosho, mazao ya chakula na kadhalika, lakini pia pale Lindi Serikali inayo ajenda ya Mradi wa *LNG*. Hivyo uwanja huu ni muhimu sana acha utalii pamoja na mambo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutambua hilo Serikali hii ya Dkt. Samia Suluhu Hassan imeamua kuujenga uwanja huu na hatua zifuatazo zimekamilika; kwanza kukamilisha usanifu, lakini pili tulikwishatangaza na kumpata mkandarasi lengo ni kujenga uwanja mkubwa wenye hadhi na wa kisasa utakaogharimu zaidi ya shilingi bilioni 120 na kwa sasa tunachokizungumza ni kutafuta fedha za malipo ya awali ili mkandarasi alipwe na aanze kujenga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimuombe Mheshimiwa Mbunge awe na subira kipindi ambacho michakato ya ndani inakamilika na hatimaye tuweze kuanza ujenzi wa uwanja huu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mustapha Kawamba.

**MHE. JUMA M. KAWAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi kuuliza swali la nyongeza kwenye hii Wizara ya Uchukuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kuipongeza Wizara kwa kusimamia sekta ya uchukuzi nchini, lakini pili nilikuwa naomba kuuliza swali langu, naipongeza Serikali kwa jitihada ambazo imeendelea kufanya kwa ujenzi wa reli ya *SGR* kutoka Dar es Salaam – Morogoro mpaka sasa hivi iko Dodoma lakini hasa kwenye kuanza *lot* mpya ya kuanzia Makutupora kwenda

mpaka Tabora na mikoa mingine ambayo ni kilometa 368... *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kawamba, unauliza swali la uwanja wa ndege, sasa hivi tuko kwenye uwanja wa ndege. Kwa hiyo, kama una swali la *SGR* inabidi uliweke kama swali la msingi. Sawa?

**MHE. JUMA M. KAWAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa haya, Mheshimiwa Waziri nashukuru kwa majibu hayo.

Waheshimiwa Wabunge, tunamalizia swali la mwisho Mheshimiwa John Stephano Luhende, Mbunge wa Bukene, aulize swali lake.

Na. 529

**Kampuni ya Yapi Merkezi Kulipa Fidia Nzega**

**MHE. JOHN S. LUHENDE** aliuliza:-

Je, lini Kampuni ya Yapi Merkezi wanaojenga Mradi wa *SGR* Bukene italipa fidia ya shilingi 2,666,666,666.64 inazodaiwa na Halmashauri ya Nzega?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Uchukuzi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa John Stephano Luhende, Mbunge wa Bukene kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kampuni ya Yapi Merkezi inayojenga Mradi wa Reli ya Kisasa kipande cha nne (Tabora hadi Isaka). Imeshaanza utekelezaji wa makubaliano yao ya tozo za madini ujenzi yanayotumika katika ujenzi wa reli ya kisasa kipande cha nne husuani kwa madini ujenzi yanayotwaliwa na kutumika

kutoka katika machimbo zilizo chini ya usimamizi wa Wilaya Nzega Vijijini kama ifuatavyo; mnamo mwezi Machi, 2026 Kampuni ya Yapi Merkezi imelipa jumla ya fedha za Kitanzania shilingi 66,000,000 ikiwa ni awamu ya kwanza ya malipo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awamu ya pili ya malipo ya tozo za madini ujenzi kiasi cha fedha za Kitanzania shilingi 136,000,000 inalipwa mwezi Mei, 2026, ikifuatiwa na malipo ya awamu ya tatu ya jumla ya fedha za Kitanzania shilingi 136,000,000 ambayo inalipwa mwezi Julai, 2026; na kisha malipo ya tozo za madini ujenzi yenye thamani ya fedha za Kitanzania shilingi milioni 136.7 yataendelea kufanyika kila mwezi kuanzia mwezi Oktoba, 2026 hadi mwezi Machi, 2028.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa John Stephano Luhende, swali la nyongeza.

**MHE. JOHN S. LUHENDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, kwanza ahsante sana kwa Serikali kwa kulishughulikia suala hili naona kwa sasa tumeanza kupokea fedha zinazotokana na madini ujenzi ndani ya halmashauri yetu. Maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza kumekuwa na changamoto nyingi kwa wakandarasi kutolipa fedha hizi kwa wakati. Kwa nini Serikali isiweke utaratibu wa kuwa inazikata fedha zile moja kwa moja kabla ya kumlipa mkandarasi na kuzielekeza kwenye halmashauri husika? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kumekuwa na changamoto ya wakandarasi kuja na wafanyakazi wao hasa wafanyakazi wa kawaida kama wale wanaotumika katika kufyeka, kukata miti na kazi nyingine za ujenzi ndogo ndogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini Serikali msiweke msisitizo wa kuhakikisha kwamba wanapokuwa wanatekeleza miradi kwenye vijiji husika watumike wananchi wa vijiji hivyo ili tuweze kutengeneza ajira pamoja na kuinua uchumi wa eneo hilo? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Uchukuzi, napenda kumjibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa John Luhende kama ambavyo ameuliza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza ametoa kama ushauri kuhusiana na kwa nini tusione umuhimu wa kukata moja kwa moja? Na kabla sikujibu swali lake kwa niaba ya Serikali nipokee pongezi zake ambazo amezitoa kwa hii Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan jinsi inavyosimamia na kuratibu kwa umakini mkubwa mradi mkubwa kwenye nchi yetu wa *standard gauge*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia nimrejeshee pongezi yeye mwenyewe kwa kuthibitisha umakini na ujasiri wa kufuatilia na kusimamia maslahi ya Watanzania, lakini hasa wa jimboni kwake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakubaliana na ushauri wake na Serikalini tumekwishaanza kufanyia kazi ili ikiwezekana wale wakandarasi ambao watakuwa na changamoto pengine za kulipa malipo hayo kwa wahusika au kwa vibarua tuone namna bora ya kulifanyia kazi jambo hilo bila kuathiri sheria, kanuni na taratibu za nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nitumie nafasi hii kutoa rai kwa wakandarasi wote waliopo kwenye sekta yetu Mheshimiwa Waziri anatoa maelekezo kwamba ni vyema wakazingatia mikataba wanayoingia na Watanzania ili Watanzania wanaopata fursa ya kufanya kazi kwenye maeneo hayo basi waweze kulipwa stahiki zao kwenye nchi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; Mheshimiwa Mbunge anatoa msisitizo kwamba ni vyema vipaumbele vitolewe kwa wananchi waliopo kwenye eneo hilo kabla ya kwenda maeneo mengine; hapa kwanza nikubaliane naye kipaumbele siyo upendeleo ni jambo la muhimu kwamba kama mradi unatekelezwa katika eneo hilo basi ukiwa na vijana wenye sifa kwenye eneo hilo wapewe kipaumbele zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili haimanishi kwamba kukiwa na mradi sehemu "A" basi wananchi wa maeneo mengine wasipate fursa hiyo hiyo kwa sababu tukifanya hivyo sasa nchi yetu tutaiingiza mahali pabaya zaidi. Maana yake kule kusipo na migodi basi Watanzania wasiajiriwe waajiriwe wa hapo hapo, kule kusipo na bandari, kule kusipo na uwanja wa ndege na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunachokisema tutatoa fursa kwa Watanzania wote, lakini ikiwezekana wa eneo hili hususan kwa kazi kama za vibarua waweze kutazamwa zaidi ili waone na wao wananufaikaje katika eneo lao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Paschal Chinyele, Mheshimiwa Kawamba Mustafa ajiandae.

**MHE. PASCHAL I. CHINYELE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, wakazi wa Kata za Kikuyu Kusini, Mkonze pamoja na Zuzu ni miongoni mwa Watanzania waliopata bahati ya kupitiwa na reli ya *SGR*. Hata hivyo, iko changamoto kubwa ambayo imepelekea wakazi hawa kushindwa kuvuka kutoka upande mmoja kwenda mwingine kujitafutia riziki hasa maeneo ya mjini.

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga madaraja ya juu hasa zinaitwa *overpass* ili wakazi hawa waweze kuvuka kirahisi na hususan eneo la Michese katika Jimbo la Dodoma Mjini ambalo lina wakazi wengi sana walau wajengewe *overpass* moja tu waweze kupita maana sasa wanajua kutembea hadi kilometa nne ili kuvuka upande wa pili.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Uchukuzi napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Chinyele, Mbunge wa Dodoma Mjini ambaye ametaka kufahamu mpango wa Serikali katika kujenga madaraja ya juu, vivuko vya juu katika maeneo mbalimbali ili kusaidia wananchi wake wa Kikuyu Kusini, Michese, Mkonze, Zuzu na maeneo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nampongeza, ni Mbunge ambaye ndiyo ameingia kwa mara ya kwanza, lakini unaweza kuona jinsi ambavyo anakesha kupambana na kupigania wananchi wa jimbo lake. Kweli nampongeza sana kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wetu na hata Waziri pale huwa anamsumbua sana kila wakati anaenda pale, mara amemwambia habari za Kizota mara Zuzu na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili nataka pia kumjibu Mheshimiwa Mbunge kwamba kwanza uwekaji wa madaraja au vivuko vya chini na juu vinafanywa kwa kuzingatia sheria, taratibu na kanuni na kwa kawaida vinapangwa kabla mradi haujaanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa hivi tunapozungumza, kuanzia Dar es Salaam mpaka Kigoma na mpaka Mwanza tayari Serikali ilikwishatambua maeneo ambayo yanapaswa kuwekewa vivuko hivyo. Kwa kuwa ameleta hoja hii mpya, ninawaelekeza Shirika la Reli waende wakaangalie maeneo hayo na kutazama, kulinganisha na mipango iliyopo Serikalini ili kama linawezekana basi tuone namna bora ya kuweza kulifanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu pia ni changamoto, ni vigumu kusema kwamba kila palipo na watu tukaweke daraja la juu, kwa sababu ni gharama kubwa sana, lakini ushauri wake tumeupokea na ninaamini Mkurugenzi wa Shirika la Reli atakwenda kulitazama eneo hilo, na baada ya hapo chini ya maelekezo ya Mheshimiwa Waziri tutaona namna bora ya kuweza kufanyia kazi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mustafa Kawamba, swlai la nyongeza.

**MHE. JUMA M. KAWAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kunipa nafasi niulize swali la nyongeza kwenye Wizara hii ya Uchukuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninapenda kuipongeza Serikali kwa kuanza kujenga kipande cha *Lot 3* kutoka Makutupora kwenda Tabora na mikoa mingine, chenye kilometa 368.

Swali langu linajielekeza hapa, je, ni lini treni yetu ya gari moshi ambayo inabeba mizigo pamoja na abiria itaanzisha safari zake za kutoka Dar es Salaam – Morogoro – Dodoma mpaka kufika Tabora ili wakazi wa Vijiji vya Tura, Mayongwe, Nyahua, Goweko na Igalula waweze kunufaika kusafirisha abiria pamoja na mizigo ndani ya Jimbo la Igalula? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mustafa, Mbunge wa Igalula kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaamini anamaanisha treni ya kisasa kwenye reli ya kisasa, kwa sababu kama ni treni ya *metre-gauge* inafanya kazi japo kwa kusuasua. Kwa sababu hiyo, kwanza nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, dhamira ya Serikali ni kuhakikisha kwamba nchi yetu inaendelea kunufaika kupitia sekta yetu ya uchukuzi kwa kuboresha njia ambapo kwa sasa njia ya treni ya *metre-gauge* njia yake inaendelea kuboreshwa kutokana na kwamba uwezo ulishuka sana, awali ilikuwa ni kubeba mzigo tani milioni tano, ukashuka mpaka tukafikia asilimia tano. Kwa hiyo, kwenye vipande mbalimbali Serikali inaendelea kufanya maboresho hayo makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, kwenye upande wa reli ya kisasa ya *SGR*, Serikali imekwishaweka wakandarasi. Wote wako kazini, kutoka Dar es Salaam mpaka Kigoma, kutoka Tabora mpaka Mwanza. Mradi huu wote utaigharimu Serikali takribani dola bilioni 11.2.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa habari njema zaidi, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan mpaka ninapozungumza amekwishalipa zaidi dola bilioni 4.8 na wakandarasi hao wanadai kiasi kidogo cha fedha na wengine wanaendelea kutekeleza majukumu yao, watakapokamilisha wataendelea kulipwa, ninaamini kwamba mara baada ya mradi huu kukamilika basi wananchi wa Igalula, Mkoa wa Tabora pamoja na maeneo mengine nao wataanza kunufaika moja kwa moja na reli yetu au

na treni yetu ya kisasa kama vile ambavyo kutoka Dar es Salaam mpaka Morgoro, Morogoro mpaka Dodoma tunavyonufaika.

**MWENYEKITI:** Tunamalizia na Mheshimiwa Kenneth Nollo.

**MHE. KENNETH E. NOLLO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona Serikali ikiweka Bandari Kavu sambamba na *SGR* na tumeona imefanya vizuri kuanzia Bahi na Isaka, lakini ukiangalia mizigo mingi inayoenda nje ya nchi inapita njia ya Tunduma.

Je, Serikali haioni kwamba iweke Bandari Kavu Morogoro ili mizigo mingi inayoenda *corridor* ya Tunduma kwenda Zambia na Kusini mwa *DRC* iweze kuchukuliwa kiurahisi katika sehemu ya Morogoro? Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, kama linawiana na hilo la *SGR*, ninaomba majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Kenneth Nollo, Mbunge wa Bahi ambaye ninampongeza kwa jinsi anavyotazama umuhimu wa kuboresha sekta yetu hii ya Uchukuzi kwa sababu ndugu Waheshimiwa Wabunge, tukikubaliana sisi sote kwamba tukiboresha sekta yetu hii ya uafirishaji, kwa maana ya kujenga uwezo wa kibandari sambamba na miundombinu yake, basi nchi yetu ina nafasi ya kufanya vizuri zaidi katika ukanda wetu huu wa Kusini mwa Afrika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Serikali inatambua umuhimu wa eneo la Morogoro na ninamhakikishia, wenzetu wa *TRC* (Shirika la Reli) wanayo maeneo ambayo walikuwa wameshayatenga. Ninaamini kwa ushauri huu tunaupokea na kuanza kuuchakata ili ama kushirikisha sekta binafsi kuhakikisha ya kwamba tunajenga bandari kavu kubwa. Kwa kweli kama anavyosema, mzigo mkubwa unakwenda Kusini mwa Afrika kuanzia na nchi zetu za jirani. Kwa hiyo, ukiwa na Bandari Kavu

kubwa pale Morogoro, ni kweli itarahisisha mzigo wa *SGR* ukaja mpaka Morogoro, halafu pengine magari yakachukulia pale kwenda kwenye mikoa hii ya Kusini sambamba na nchi jirani ikiwemo Zambia, Malawi na nchi nyingine. Kwa hiyo, ni ushauri mzuri ambao Serikali tunaupokea.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu hayo kwa Waheshimiwa Wabunge kwa Wizara ya Uchukuzi.

Waheshimiwa Wabunge, tumemaliza kipindi chetu cha maswali na sasa tuna matangazo hapa. Nitaanza na matangazo ya wageni walioko Bungeni asubuhi hii.

Wageni ambao wamekaa Jukwaa la Spika, tuna wageni 14 wa Mheshimiwa Emmanuela Kaganda Mtatifikolo ambao hao ni familia yake kutoka Ismani Mkao wa Iringa. Yupo Mheshimiwa Balozi CP. Suzan Kaganda, Balozi wa Tanzania nchini Zimbabwe na wifi wa Mheshimiwa, karibu sana. *(Makofi)*

Yupo pia Ndugu Constantine Kihwele, Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Iringa Vijijini, karibu sana. *(Makofi)*

Pia yupo Ndugu Lena Hongole, Mwenyekiti UWT Wilaya ya Iringa Vijijini, karibu sana. *(Makofi)*

Mgeni mwingine ni Ndugu Arnold Mvamba, Mwenezi Iringa Vijijini, karibu. *(Makofi)*

Yupo pia Ndugu Solomon Kasaba, Mratibu wa Uchaguzi Jimbo la Ismani, karibu sana. *(Makofi)*

Pia yupo Ndugu Ponsiano Kayage, Meneja wa Kampeni Jimbo la Ismani, karibu sana. *(Makofi)*

Mgeni mwingine ni Ndugu Wili Mongo, Mzee maarufu Jimbo la Ismani, karibu sana. *(Makofi)*

Pia Ndugu Amos Ndaso, Katibu wa Mheshimiwa, karibu sana. *(Makofi)*

Yupo Ndugu Vedasto Rweimamu, baba mlezi wa Mheshimiwa, karibu sana. *(Makofi)*

Pia yupo Ndugu Liberata Kiseo, mama mdogo wa Mheshimiwa, karibu sana. *(Makofi)*

Wapo pia Ndugu Dennis Mtatifikolo, kaka wa Mheshimiwa na Ndugu Obed Mtatifikolo, kaka wa Mheshimiwa na Dkt. Agnes Kaganda, wifi wa Mheshimiwa. *(Makofi)*

Kuna wageni wengine 17 wa Mheshimiwa Emmanuela ambao ni ndugu jamaa na marafiki kutoka Jimbo la Ismani. *(Makofi)*

Karibuni wageni wote wa Mheshimiwa Mbunge wetu wa Ismani katika Bunge letu la Jamhuri ya Muungano. *(Makofi)*

Wageni wengine ni wageni wa Waheshimiwa Wabunge; wageni 20 wa Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko, Mbunge ambao hawa ni Wanakwaya wa Kanisa la Waadventista Wasabato kutoka Msonga, Bukombe, Mkoani Geita, karibuni sana Wanakwaya kutoka huko Geita. *(Makofi)*

Wageni 37 wa Mheshimiwa Dkt. Jafar Rajab Seif, Mbunge na Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ambao hawa ni viongozi wa Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi UVCCM, kutoka Mkoani Geita. Karibuni sana viongozi wetu wa UVCCM kutoka Geita. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Edwin Enosy Swalle, familia yake kutoka Jijini Mbeya, karibuni sana wageni wetu. *(Makofi)*

Wageni 23 wa Mheshimiwa Dkt. Balozi Pindi Chana ambao hawa ni wakulima wa kutoka Kata ya Mundindi, Mkoani Njombe. Karibuni sana wageni wetu kutoka Njombe. *(Makofi)*

Wageni sita wa Mheshimiwa Neema William Mgaya ambao ni wafanyabiashara *Live to Love Group* kutoka Jijini Dar es Salaam, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni 20 wa Mheshimiwa Haran Nyakisa Sanga, Madiwani na viongozi wa CCM kutoka Wilaya ya Kigamboni Jijini Dar es Salaam, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni 73 wa Mheshimiwa Zainab Abdallah Issa, wanafunzi na walimu wa Shule ya Awali na Msingi *Deep Sea* kutoka Jijini Dar es Salaam. Kati ya hao, watoto Tauhida Akulene na Opthmani Akulene ni watoto wa Mheshimiwa Jamila Juma. Karibuni sana wanafunzi kutoka *Deep Sea,* Dar es Salaam. *(Makofi)*

Kuna wageni wengine ambao wametembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo, Ndugu Kennedy Musaba, mwanafunzi wa Ndaki ya Tiba kutoka Chuo Kikuu Dodoma *(UDOM)*, karibu sana. *(Makofi)*

Yupo pia Ndugu Teresia Mwendapole, Afisa Maendeleo ya Jamii kutoka Jijini Dodoma, karibu sana. *(Makofi)*

Wageni 41 kutoka Kikundi cha *Bravo Women* cha Jijini Dar es Salaam, karibuni sana Kikundi hicho cha *Bravo Women* kutoka Dar es Salaam. *(Makofi)*

Pia tuna timu ya wanamichezo 25 wa *Albinism Sports Club* kutoka Kinondoni Jijini Dar es Salaam, karibuni sana. *(Makofi)*

Tangazo lingine ni tangazo kutoka kwa Katibu wa Bunge; anawaomba Waheshimiwa Wabunge kwamba siku ya Jumamosi tarehe 6 Juni 2026 kutakuwa na mchezo wa kirafiki kati ya Timu ya Mpira wa Miguu ya *Bunge Sports Club* na Timu ya Watu Wenye Ualbino *(Albinism Sports Club)* kutoka Dar es Salaam, ambapo mchezo huo utachezwa saa 10.00 jioni katika Kiwanja cha Jamhuri Dodoma.

Hivyo Waheshimiwa Wabunge wote mnaombwa kufika bila kukosa ili kushiriki na kutia hamasa ya ushindi katika mchezo huo muhimu.

Waheshimiwa Wabunge, haya ndiyo matangazo yetu kwa leo na kwa vile tumemaliza shughuli zetu zote za leo, ninaahirisha Shughuli za Bunge hadi kesho saa 3.00 asubuhi.

Samahani, ninaahirisha Shughuli za Bunge hadi siku ya Jumatatu saa 3.00 asubuhi. *(Kicheko)*

*(Saa 5.09 Asubuhi Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Jumatatu, Tarehe 8 Juni 2026, Saa Tatu Asubuhi)*